

UFUNUO, MLANGO WA TANO

SEHEMU YA II

 ...kurudi maskanini asubuhi ya leo, na kutangaza habari njema kote, jinsi ambavyo Bwana Mungu amekuwa mwema kwetu.

² Jumapili iliyopita wakati ono lilipoelezewa, na karibu ninyi nyote mlikuwa hapa (kuhusu kuuawa kwa yule nyoka kule kwenye kituo): ono hilo lilitukia neno kwa neno katika saa ishirini na nne baada ya kusimuliwa hapa jukwaani. Ilikuwa ni tukufu jinsi Bwana alivyolifanya. Sijawahi kuona moja ya hayo likishindwa katika ... maishani mwangu mwote, nami nina umri wa miaka hamsini na miwili. Kikamilifu kabisa, neno kwa neno jinsi lilivyotukia. Nami ninajisikia vizuri zaidi, vizuri zaidi.

³ Na sasa kuna hayo yote niliyokuwa nikinena habari zake, nikisema kuhusu lile shtaka. Ama, sio shtaka, ilitoka kwa watu wenye mioyo miaminifu, wanaomcha Mungu, ambao huduma yangu ilikuwa tu imekuwa kidogo ni ya kimbi-...kimbinguni kupita kiasi, nao walikuwa wameanza kuwaza ya kwamba nilikuwa Bwana Yesu, na hiyo inasaba-...ikaanzisha fundisho dogo kuhusu jambo hilo. Bali lote lilikomeshwa mara moja. Bwana ashukuriwe kwa ajili ya jambo hilo!

⁴ Na mara tu mimi mwenyewe nilipotoka kwake na kumwacha tu Bwana alichukue na nikalikabidhi kwa Bwana, liliisha mara moja, chini ya saa ishirini na nne lilikuwa limekwisha. Liliniacha kidogo nina wasiwasi na kufadhaika kidogo, lakini litaniondokea baada ya kitambo kidogo. Hakika kidogo lilinishtusha sana, bali niko sawa na bora sana.

⁵ Nasi tulikuwa na ushindi mkuu sana juma hili, ninataka kutoa taarifa ya jambo fulani.

⁶ Sasa, kama ningalisikiliza yale Bwana aliyoniambia, hilo kamwe lisingaliibuka. Miaka minne iliyopita Yeye aliniambia. Naye mke wangu aliyepo hapa, nyuma kwenye wasikilizaji hapa mahali fulani sasa, naye mwanangu ameketi... alikuwa hapa jukwaani dakika chache zilizopita, na wengine wengi walionisikia nikisema mara kwa mara, "Huu ndio wakati wa mwisho nitakapokuwa na wowote wa upambanuzi huo." Mnaona? Ilifikia kwamba... Nilijaribu kuishi karibu sana na Mungu, na, katika kufanya hivyo, ndipo linasababisha kitu fulani kinachowafanya watu kidogo kuchanganyikiwa hata karibu hawajui la kuwazia.

⁷ Halafu basi, kwenye ile kesi ya kodi tuliyokuwa nayo, kusingalikuwako na neno moja kuihusu hiyo kama tu

ningalimsikiliza Bwana. Sikuzote ni pale ninaponinii... Ambapo simtii Yeye ndipo sikuzote ninaingia kwenye shida. Laiti ningalisikiliza kwa makini na kutembea pamoja na Yeye!

⁸ Halafu inafikia... Hii huduma ni ya kimbinguni sana wakati mwingine hata mimi... Nilihofia nitaingia kwenye mstari ule mwingine. Lakini, sasa, simaanishi... ninataka kuninii... kila mmoja, kulipata hili vizuri, ya kwamba simaanishi kusema kwamba ninaondoka, nitamwacha Bwana, bali sitaki tena kudhihirisha yoyote ya kimbinguni, mnaona, kwa hiyo kwa njia kama vile upambanuzi na—na mambo kama hayo.

⁹ Sasa, Bwana ameturehemu kwenye wakati huu; Yeye amemwinua Ndugu Neville, ambaye ana neno la unabii; Yeye anaye Ndugu Higginbotham na wengine wengi wa hao ndugu wengine hapa ambao kabisa ni... kupitia kwa karama za kiroho kanisani, wanafanya miujiza.

¹⁰ Basi hebu niwapeni tu ushuhuda. Kulikuwako na Dada Opal Weaver, sijui kama yeye yuko pamoja nasi hapa kanisani asubuhi ya leo ama la. Uko hapa, Dada Opal? Ambapo huenda nisiweze ku—kumwona. Loo, vema, miaka kadhaa iliyopita alikuwa yuafa kwa kansa, nayo hiyo kansa ilikuwa kwenye tezi ya kike kisha ikaingia kwenye mafigo yake. Ndipo wakampa usiku huo mmoja ya kuendelea kuishi, alikuwa amedhoofika sana. Basi nikaenda nikamwombea, ndipo ono likaja, naye akaponywa kabisa. Na hiyo imekuwa yapata miaka kumi na mitano iliyopita. Alikuwa na kutoka miongoni mwetu kwa miaka na miaka.

¹¹ Hivi majuzi alishikwa na ugonjwa ambapo alikuwa... alikuwa na maumivu mabaya sana ya koo hata akaanza kutokwa na damu kwenye koo lake. Ilipendekezwa kwamba amwone daktari mara moja. (Na hapo ni wakati nilipokuwa Canada.) Basi akampigia simu Ndugu Neville, naye Ndugu Neville akaenda akamchukua Ndugu yetu Higginbotham. Sidhani Ndugu Higginbotham yuko hapa, huenda akawa, asubuhi ya leo. Ndugu Rupert Higginbotham alikuwa mmoja wa wadhamini wetu wa zamani, ndugu mzuri. Yupu hapa? Kwa hiyo wapakanda kwenda kumwombea mwanamke huyo, ndipo walipomwombea... Alikuwa akitokwa na damu sasa, sijui ni muda gani, kwa siku kadhaa, siku mbili ama tatu, naye akaendelea tu kutema damu. Naye Ndugu Neville akamwombea wala hakutema tone moja zaidi la damu. Hiyo ni kweli.

¹² Halafu alikuwa na vivimbe viwili, mabaka ama chochote kile kwenye kilele cha kinywa, kitu kama uwati ama chochote kile kilichoning'inia kwenye kilele cha kinywa chake; vivimbe vikubwa, kitu kama hicho. Wala hakuwa amepata nafuu hata kidogo kutoka kwake, navyo vilikuwa... Akasema, "Vilikuwa yapata ukubwa nusu ya kokwa ya hikori." Navyo vilikuwa kinywani mwake kwa—kwa muda, siku kadhaa. Naye Ndugu

Higginbotham...Kwa vile silitamki jina hilo la Kijerumani vizuri sana, Ndugu Rupert, nisamehe kwa jambo hilo. Lakini hata hivyo, mimi...Nami huenda nikalikosea hili papa hapa. Ama, la, ninaamini a—anayo karama ya kunena kwa lugha na kufasiri lugha. Naye alikuwa ameuweka mkono wake, kwenye wakati huu, juu ya uso wake. Ndipo akasema, “Ndugu Branham, sio jana, sio usiku wa jana, bali mara mahali hapo pakaondoka” kutoka kwenye kilele cha kinywa chake. Mara moja!

¹³ Kisha hao madaktari wakaja, wakaangalia kooni mwake, na kila kitu, nao wakasema, “Hana budi kwenda hospitalini maana ana kansa ya koo.”

¹⁴ Kwa hiyo sisi...Wakampeleka hospitalini. Nami hata sikujua alikuwa hapo ndani mpaka nilipokutana na mchungaji wetu mwema, Ndugu Neville, hapa juu, nami nilikuwa nikienda zangu hospitalini naye akaniambia ya kwamba—ya kwamba alikuwa pale. Kwa hiyo nikapanda kwenda kumwona, naye mume wake alikuwa ameketi pale. Basi madaktari watano, wanne ama watano, walikuwa wamekuja na kumfanyia uchunguzi, huku wakivitikisa vichwa vyao, wakasema, “Ni, kweli, ni kansa, kansa ya virusi, ni kansa.”

¹⁵ Kwa hiyo daktari mwanagenzi akaingia naye akachukua sa—sampuli yake. Akasema, “Hiyo, bila shaka, ni kansa.”

¹⁶ Nami nikasema, “Lakini, dada, kama Mungu alikuponya kansa wakati mmoja...hata iwe ni nini. Huenda ikawa watu hao wanasema kweli. Wao ni—wao ni watu waliofunzwa katika fani hiyo kujua kama ni kansa ama inaonekana kama kansa ama chochote ilicho. Hiyo ni...Hao ni watu waliofunzwa kwa kusudi hilo. Nayo inaonekana kama kansa kwa hiyo wanasema ni kansa.” Ndipo nikasema, “Huenda ikawa ndiyo.”

¹⁷ Lakini yeye hakutaka kuamini ilikuwa ni kansa. Kwa hiyo, nikasema, “Lakini kama Mungu angeweza—angeweza kujibu maombi pale juu na kukomesha kule kutokwa na damu; Mungu angeweza kujibu maombi, aviondoe vitu hivyo vikubwa kinywani mwako. Hata iwe nini, hivi Mungu hawezi kuikomesha papa hapa?”

¹⁸ Akasema, “Amina!” Naye mumewe ameketi pale. Naye akasema, “Hilo ndilo ninalotegemea sasa hivi, kwamba Mungu ataikomesha.”

¹⁹ Ndipo nikamwombea. Basi wakazipeleka sampuli hizo kuchunguzwa, nazo zikarudi “haipo” wakati wote walisema ilikuwa ni *kansa*. Mnaona?

²⁰ Kwa hiyo jambo ni kwamba, enyi marafiki, kwamba Yeye ni Mungu na Yeye huyajibu maombi. Nasi tuna furaha sana kwamba Yeye hutuzuru hapa kwenye maskani hii nyenyekevu. Haionekani ya kuvutia macho, maskini mbao tulizoweka pamoja hapa, miaka mingi iliyopita, tupate kinga juu ya kichwa chetu, paa juu ya kichwa chetu, hasa, kutokana na mvua na theluji na

kadhalika. Lakini watu wengi wanaishi leo hii kwa sababu ya jitihada hizi, na kwa hilo tunashukuru sana.

²¹ Tunashukuru kwa ajili ya wadhamini wetu. Tunashukuru kwa ajili ya mashemasi wetu. Tunashukuru kwa ajili ya kusanyiko letu. Na tunashukuru kwa ajili ya mchungaji wetu. Tunashukuru kwa ajili ya kila karama ambayo Yeye ametupa humu kanisani. Nasi tunaomba ya kwamba Yeye atawapa wanaume hawa ufahamu, kwamba kamwe hawataenda kando upande usiofaa bali watakaa moja kwa moja katikati ya barabara pamoja na Hilo. Kamwe wasijikweze wala chochote kile; ufanyapo hilo, umekwisha papo hapo, unaona. Dumu tu mnyenyekevu na Hilo.

²² Kisha mnaona, sasa, halafu watu wakiingia, wagonjwa na wanaoteseka, wapate kuombewa wakati nikipumzika sasa kwa labda mwaka mmoja ama miwili, basi Mungu ameweka njia ya kulishughulikia wakati nikimpuzika kidogo. Mnaona? Loo, hiyo si ni shukrani? Inapaswa . . . Tunapaswa kushukuru kwa ajili ya jambo hilo? Mungu kamwe hajiachi Mwenyewe bila shahidi, na kwa hiyo tunafurahia hilo sana.

²³ Sasa, juma hili lijalo, Bwana akipenda, ninapaswa kuwapeleka wasichana wangu wadogo ambao ndio kwanza watoke shuleni kwa likizo yao ndogo ya shule, kwa hiyo ninaomba kwamba mtatuombea. Binti yangu mkubwa, kwenye shule ya sekondari ya juu, anataka kuona mahali ambapo Paul Revere aliendesha farasi wake usiku wa manane, ambapo aliondoka kanisani pale. Nasi . . . Ni papa hapa New England nasi tunataka kupanda huko tukapaone.

²⁴ Halafu, daima nimetamani kuona Old Ironsides. Ni wangapi waliopata kusikia juu ya ule ushairi wa *Old Ironsides*? Ndio ninaopenda sana kati ya wote nijua; nje ya ule wa Kikristo, huo ndio mzuri sana kwangu. Ninaninii tu . . . Nikianza kuyasoma ninasongwa na kuketi chini, ninatembea kote, ninarudi. Ungewezaje kuuzamisha baada ya . . . Ni kama tu kumchukua farasi na kumwua akiisha kukupatia riziki wewe na familia yako. Kamwe—kamwe siwezi kuona hilo. “Kwa hiyo nitamwangamiza!” La, usifanye hivyo. Wakati risasi za mizinga ya Waingereza zilipolipiga na kurushwa nyuma kutoka kwenye kuta zake za mwaloni, ni—nisingeweza kukuona ukimtoa nje na kumzamisha.

Kumkabidhi kwa miungu ya dhoruba,
Radi na dhoruba!

Ninayapenda hayo sana.

²⁵ Kisha tunataka kushuka tuje, wala Bw. Kennedy hajatualika, bali kweli tunataka kuiona Ikulu wakati tukiwa kule. Wao . . . Nimekuwa mle mara kadhaa bali watoto wanataka kuiona. Kisha tutarudi nyumbani, Bwana akipenda. Kwa hiyo tuombeeni.

26 Nasi tunawaombea wapendwa wetu wote hapa walio likizoni, wengi wao wakifanya safari zao kwenda sehemu mbalimbali. Na baadhi yao wameondoka asubuhi ya leo, huko chini Kentucky na Tennessee na sehemu mbalimbali. Kwa hiyo tunawaombea.

27 Sasa, kulikuwako na jambo lingine nililotaka kutangaza. Loo, naam, ibada ya ubatizo ni mara baada ya ibada hii. Halafu basi—basi ninaamini kutakuwako na kuweka wakfu watoto wachanga, huyu ndugu alikuwa akiniambia habari zake, kuwaweka wakfu watoto wachanga. Na mambo mengi sana tunayopaswa ku-...Ati nini? [Mtu fulani anamuuliza Ndugu Branham kuhusu ibada ya jioni—Mh.] Vema, sijisikii kuchukua ibada zote mbili. Mnaona, ninachukua moja na Ndugu Neville anachukua hiyo nyingine. Nami siwezi...Sio...Wakati sisi wawili tukiwapo hapa, kwa nini kumchosha mmoja wetu? Hiyo si ni kweli, Ndugu Neville? Hiyo ni kweli kabisa.

28 Na, halafu, Doc aliniambia niku-...niwaambie ninyi nyote mzikumbuke, ahadi zenu kwa maskani, kwamba—kwamba hili kanisa...ya kwamba wanawazia kujenga mara wawezapo kukusanya za kutosha kwa ajili ya kanisa.

29 Na kwa hiyo ni—nilikuwa...Ilionekana kwangu kana kwamba kulikuwako na jambo fulani, hapana shaka ilikuwa ni wakati uliponiambia juu ya hilo, kuwekwa wakfu kwa watoto wachanga. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Nasi tutakuwa na hiyo mara baada ya kumaliza ibada hii sasa.

30 Sasa, hizi ni za kuombewa, nguo, nadhani? Vema, bwana. Tutafanya hivyo pamoja, na kisha...

31 Sasa, kabla hatujalikaribia Neno...Ni wangapi hulifurahia Neno? Loo, jamani, kuishi mlimani! Mnaona, m—mngeweza kuona tangu Jumapili iliyopita kinachomaanisha kufanya mapenzi ya Mungu. Mnaona? Nilipoona hiyo ilikuwa ni roho iliyokuwa imeingia miongoni mwa ndugu hao wa thamani, hakukuwako na njia ya mtu wa kawaida kuliondoa hilo. Kwa hiyo jambo pekee lililotupasa kufanya lilikuwa ni kuiweka wakfu ama kuikabidhi kwa Bwana, ndipo saa chache yote ikamalizika.

32 Sasa, mchungaji (nami nikiondoka), akiwa ndiye msaidizi wenu hapa katika kazi ya Bwana, na kama vile Paulo angesema, "Ninakuagiza mbele za Mungu na malaika wateule," unaona. Na kwa kanisa hili hapa, kuna mfano mkamilifu wa jambo la kufanya kama mtu akikiuka utaratibu kanisani. Mnaona?

33 Sasa, kama jambo fulani likitokea kanisani ambalo si sahihi, basi hebu mtu huyo, ambaye anajua hilo si sahihi, amwendee huyo mtu. Na kama mtu huyo hatapatanishwa; basi jambo lingine la kufanya ni kumchukua shahidi waende, ama labda shahidi mmoja ama wawili, nao wamwendee mtu huyu wapate kuwapatanisha ama kulinyosha jambo hilo. Sasa, sikilizeni kwa

makini! Sasa, hili linarekodiwa, pia. Na halafu ikiwa hilo halitafaulu...

³⁴ Kamwe msiache itikadi ndogo, ama kitu fulani kingine kidogo, maskini hisia mbaya kamwe iibuke miongoni mweni. Iondoleeni mbali mara moja! Kwa hiyo hiyo kidogo ni...Ni mbweha mdogo anayeyaharibu matofaa, mwajua. Kwa hiyo liondoleeni mbali! Hisia yoyote ya kigeni, nenda kamwambie huyo mtu kuihusu. Useme, "Ni—nimekosea. Si—sina hisia nzuri kukuhusu, ama kitu fulani. Nisaidie kuomba juu yake, kwamba nitakuwa mzuri zaidi." Kwa sababu, hatutaki chochote ila tu kabisa, Roho Mtakatifu wa Mungu asiyeghoshiwa, miongoni mwetu. Hilo tu ndilo tunalohitaji. Ndipo zile karama na kadhalika zitafanya kazi vizuri na kila kitu kitakuwa kikija sawa.

³⁵ Kwa nini kuwa na nusu kanisa wakati unaweza kuwa na zima? Kwa nini kukubali kabadala wakati anga zote zimejaa kilicho halisi? Mnaona? Hatutaki jambo hilo. Kwa hiyo kama hisia ndogo ya ajabuajabu ikiwahi kuibuka miongoni mwetu washiriki, mmoja kwa mwingine, wewe mwendee mtu huyo.

Unasema, "Vema, walinitendea..."

³⁶ Hilo...ni...Sasa, kumbukeni, sio, "kama una kosa ama hatia dhidi ya ndugu," lakini, "Kama ndugu ana neno dhidi *yako*." Mnaona? Mwendee mkapatanishwe, umwambie ya kwamba wewe—ya kwamba umekuwa na hisia ngeni kumhusu nawe unataka kufanya urafiki, kisha uombe na kushuka madhabahuni na kukiondolea mbali kitu hicho miongoni mwetu.

³⁷ Sasa, Shetani sikuzote atawapiga ngumi mpaka mtakapoisha hapa duniani. Kumbukeni tu hilo. Hutakuwa na wakati ila ambapo ngumi zinapigwa wakati wote, maana uko vitani. Hivi uliomba umjie Kristo, upate kuenda kwenye mandari? Vema, hakika utashangaa, kwa sababu ni vita sikuzote. Nimekuwa hudumani kwa muda wa miaka thelathini na mmoja, nami nimepiga vita kila inchi ya njia. Hiyo ni kweli. Ilibidi Israeli kupiga vita kila inchi ya njia. Wao—wao...Walipewa Palestina, bali iliwabidi kupigania kila inchi ya njia kuipata.

³⁸ Sasa, kumbukeni hili sasa, kwamba kama...Kwamba jambo fulani likitokea kanisani, basi hebu mchungaji...na iwapo wewe—iwapo itakubidi kuja kumchukua mchungaji, kuwapeleka kwa mtu huyo. Ndipo wasiposikia hilo, basi njoni mbele ya kanisa na kulisema mbele ya kanisa. Wape kipindi fulani cha kupatanishwa, labda kutoka Jumapili moja hadi nyingine. Na wasipolisikia kanisa, basi Biblia ilisema "Na wawe kama kafiri na mtoza ushuru."

³⁹ Kwamba, mnaona, mradi tu wamelindwa na kanisa, Shetani hawezi kuwafikia. Lakini wakati kanisa linapowaachilia watoke chini ya ulinzi wa kanisa na Damu ya Kristo, basi Shetani

ataanza kufanya kazi juu yao. Hiyo itawaleta moja kwa moja katika upatanisho tena. Mnaona? U—unaelewa hilo, sivyo, mchungaji? Naam, bwana.

40 Kwa hiyo hilo ndilo jambo la kukumbuka kufanya daima, ni kupatanishwa, njoo kwa Mungu na upitie njia ya Mungu. Tuna ninii . . .

41 Hilo linatuthibitishia nini? Wawili ama watatu wa ndugu zetu ambao wanajua ya kwamba nimejishughulisha sana chini ya huyu mwingine kwa muda wa miaka miwili ama mitatu. Hiyo ni kweli. Lakini nilipofikia mahali nilipowazia kama hao watu, nami hatimaye ningeweza kuwapenda watu hao vya kutosha hata wasingeweza kuliondokea. Nami niliwachukua mashahidi bali hilo halikufanikiwa. Ilinibidi kulileta kanisani. Ndipo basi kutoka jukwaani Jumapili iliyopita, nikasema, “Sitaki kusikia jambo hilo mara nyingine moja. Niko huru nalo. Naligeuza kwa Mungu, mnaona, na kulikabidhia Kwake tena.”

42 Ndipo mara moja inaonyesha ya kwamba watu hao walikuwa wameitwa. Hiyo . . . Sasa, endapo hawakuitwa, wakifikia masahihisho ya Kimaandiko . . . Basi mtu asiyeweza kustahimili masahihisho ya Maandiko, yeye hukasirika sana na kulipuka, inaonyesha yeye hayuko sawa na Mungu. Kweli! Bali mtakatifu halisi wa Mungu atapatanishwa na Mungu kwa Neno. Hilo ni kweli. Nalo Neno ndiyo njia ya kurekebisha. Hao ndugu wanapaswa kuwa wenye shukrani sana kwa Mungu kwamba . . .

43 Mnaona, Biblia ilisema kwamba, “Makristo wa uongo wangetokea katika siku za mwisho nao wangewadanganya walio wateule kama yamkini.” Ila haiwezekani. La, bwana. Wateule walikusudiwa tangu zamani, kwa hiyo hawatadanganyika, mnaona.

44 Kwa hiyo mara hao ndugu . . . Walikuja kule nyumbani kesho yake, mnaona, hata mpaka wakafikia na walikuwa wameanza kunipa Maandiko yao. Ndipo Roho Mtakatifu kwa Maandiko akahukumu tu kila kitu walichokuwa wakisema. Mnaona? Kwa hiyo hilo hapo, waliona, hilo kundi lililoteuliwa la watu wakaenda Mbele za Mungu. Inanifanya nishukuru kwa ajili ya watu kama hao. Naam, bwana. Hao ni watu halisi.

45 Wakati unapoweza kumwona mtu ambaye amekosea, na kuthibitishwa amekosea, basi hiyo inaonyesha yeye anataka kuwa Mkristo, anakuja huku na kusema, “Nimekosea.” Huyo—huyo ni Mkristo halisi.

46 Lakini jamaa huyo ambaye atalipuka kabisa, na kukimbia upande mmoja na kusema, “Aah, hapakuwapo na kitu chochote Kwake,” na namna hii; kuwa mwangalifu, ndugu, unaweza kuona papo hapo kwamba aliondoka chini ya hukumu kwa sababu hakuwa mmoja wetu. Lakini sikuzote, mchungaji, njoo

kwenye Neno hilo Nalo litafanya hivyo kila wakati. Ila inakubidi kudumu na Neno.

⁴⁷ Hiyo ndiyo sababu wakati ninapokuja, sasa, nina...sina utambuzi tena Ma—Marekani, kamwe sikusudii, maishani mwangu mwote, ila tu nchi za ng'ambo na kadhalika. Hakika, kama karama, kama karama ya kinabii, hiyo daima itakuwapo, lakini nitaiweka tu kwa nafsi yangu na kuifanyia kazi kwa sababu ni...tu—tumechelewa kupita kiasi sasa kwake kuninii...inazidi kuendelea. Tuko karibu mno na wakati wa mwisho. Lakini katika nchi za kigeni ni kisa kimoja tu au viwili jukwaani na, ndugu, namaanisha tayari wameondoka.

⁴⁸ Halafu tuna uigaji Wake wa kimwili. Loo, jamani! Ni huzuni tu. Angalieni, ninataka kuninii...Ni Wapentekoste wangapi waliopo hapa ndani? Inua mkono wako. Vema. Angalia, ninyi Wapentekoste, miaka michache iliyopita Mungu kweli alishuka juu yenu nanyi mkaanza kunena kwa lugha. Hiyo ni kweli. Lakini ibilisi alifanya nini? Alishuka na kutoa uigaji wa kimwili wa hilo. Akabuni kitu cha uongo, akawaangusha watu na kunena kwa lugha, akiwafanya waseme maneno fulani na vitu kuwafanya wanene kwa lugha, na kadhalika; huku mwanamume akiishi na mke wa mtu mwingine, na mambo ya kila namna, na kila namna, baadhi yao wakinywa pombe, wakivuta sigara, na kila kitu, huku wangali wananena kwa lugha. Kwa nini akafanya hivyo? Kuifanya baragumu halisi itoe sauti isiyojulikana kwa watu. Basi ni nani anayeweza kujifanya tayari kwa vita? Mnaona?

⁴⁹ Ndipo wakati hili lilipotokea...Sasa, tunao watu huko kwenye kusanyiko...Kunaye mmoja moja kwa moja... aliyenitangulia moja kwa moja huko Canada hata ninii... Mbona, makachero walimkamata kama mlawiti. Mnaona? Yeye akasema, “Mbona, Mungu alinipa karama ya utambuzi.” Kasema, “Haleluya, nina ninii...” Kasema, “Sasa, Bwana aliniambia ya kwamba mtu fulani hapa aitwaye ‘John...’”

⁵⁰ Tulikuwa na maskini mwanamke mmoja hapa asubuhi moja, aliyerudi kule, mnakumbuka, aliyerudi kule na kusema, “Bwana alinipa karama ile ile.”

Nami nikasema, “Kwa hiyo?”

Akasema, “Laiti ningalikuwa na nafasi ya kuithibitisha.”

Nikasema, “Lile pale jukwaa.”

⁵¹ Nanyi mliona lililotukia; saikolojia tupu ya umati, mnaona. Lakini mnapoona, Dada Snyder akija huku, na kumwambia yeye ana “yabisi kavu,” hilo—hilo—hilo limekwisha. Wakati Dada Synder...

⁵² Ndipo nikasema, “Hiyo siyo shida ya mwanamke huyo.” Nikasema, “Yeye alianguka na kuvunja nyonga yake.” Ndipo nikasema, “Yeye hata hasimami pale...” Hakika Dada Snyder

hakusikia vizuri sana, naye akasema . . . Basi alichokuwa nacho, ninaamini, kilikuwa ni kivimbe tumboni mwake ama tatizo lingine namna hiyo. Nikasema, “Hivyo ndivyo ilivyo; nikiketi hapa nikizungumza na ndugu kulihusu wakati huo wote.” Mnaona?

⁵³ Lakini i—inaonyesha tu ya kwamba kanisa, mnaona, ya kwamba ni uigaji wa kimwili, mnaona. Basi hilo linafanya nini? Inaifanya baragumu halisi . . .

⁵⁴ Sasa, nilipokuwa Canada walimchukua jamaa huyu aliyepanda kule. Ndipo kasema (mumo humo miongoni mwa kundi la Wanorwe), naye akasema, “Bwana ananiambia ya kwamba mtu fulani hapa ndani . . .” umati wenye ukubwa wa yapata mara kumi ya huu, “mtu fulani jina lake ‘John,’ labda ‘Johannes,’ ‘Johann.’” Kasema, “Papa hapa mahali fulani, ninaamini.” Akasema, “La,” kasema, “ni mahali fulani hapa ndani”; hakika, aliingiza ninii yote . . . Katika nchi ya Norwe? Basi kila mtu alikuwa . . . Asilimia tisini yao ni akina Petersons, Carlsons, John, Johannes, na, mbona, bila shaka. Mnaona, yeye bila shaka . . . Halina budi kuingia humo mahali fulani. Kisha, “Bwana ananiambia mtu fulani ana ugonjwa wa mgongo, ninausikia mgongo wangu ukiuma.” Mtu yeyote ambaye amelelewa kwenye Maandiko anajua ya kwamba hiyo ni saikolojia. Hiyo ni . . . Bila shaka, ndiyo.

⁵⁵ Lakini, mnaona, hiyo ilifanya nini? (Ndipo mtu huyo akakamatwa papo hapo na—na FBI kutoka hapa, walitumwa kule na kumkamata kule, Polisi Wapanda Farasi wa Kifalme.) Ndipo shirika la wahudumu likanijia, na, “Mlawiti,” wakasema, “mbona, Ndugu Branham labda ni kitu kile kile. Hivyo ndivyo tu hilo linavyoenenda, mnaona.” Linafanya nini? Kuipa baragumu sauti isiyojulikana. Mnaona? Kweli kabisa. Hivyo ndivyo ilivyo sikuzote, kujaribu kufanya mambo kama hayo kutoa sauti isiyojulikana. Hiyo ndiyo kazi ya Shetani kufanya jambo hilo.

⁵⁶ Lakini, sasa, kamwe usitofautiane na Neno hilo. Kumbuka, ninawaagiza mbele za Mungu: *Dumuni na Neno hilo!* Kamwe msitofautiane na Hilo. Basi mambo hayo yakiibuka miongoni mwa watu na vitu kama hivyo, kunalo lililo halisi kila unapoyeta la bandia. Kuna—kunayo dola bandia, hiyo inaonyesha kulikuwako na dola nzuri iliyofanyizwa kwake. Unapomsikia mnafiki fulani akinena kwa lugha, huwezi kusema yeye anaye Roho Mtakatifu. Ila, kumbukeni, yeye anaiga mtu halisi ambaye kweli ana karama ya kunena kwa lugha. Unapoyaona mambo hayo yaliyo ya uongo, kumbuka, yalifanyizwa kutoka kwa yaliyo halisi. Mungu ndiye mwanzilishi wa vitu vyote vizuri, bali Shetani huziigiza hizo karama. Vema, nikiingilia hayo, hatutaingia kwenye somo letu, sivyo?

⁵⁷ [Ndugu Ben Bryant anasema, “Ndugu Branham, samahani kidogo tu?”—Mh.]

Naam, ndugu.

[“Tafadhali? Sikuwa hapa Jumapili iliyopita, nami nilikuwa nimepata fununu ya yale uliyokuwa ukizungumzia yapata miezi michache iliyopita, nami kweli nilisumbuka juu yake, sana, na nikajisikia kuja kukwambia kulihusu na kumwambia Ndugu Neville. Lakini nilijisikia pia ya kwamba ungejua mimi na mke wangu tuliliombea. Basi asubuhi ya leo nilipokuja maskanini, sikujua yaliyokuwa yametukia, ndipo mmoja wa ndugu wa thamani akanijia asubuhi ya leo na kuniomba nimsamehe. Nami nafikiri hiyo ilikuwa ni Roho inayofanana na ya Kristo.”]

Amina.

[“Nami nafikiri ni jambo la kusifika sana kwa huyo ndugu.”]

Naam, bwana.

[“Aliniomba nimsamehe, maana alikuwa akijaribu kuninii...yeye alikuwa—alikuwa akijaribu kuniletea lile fundisho.”]

Naam.

[“Nami nisingelikubali. Basi akaniomba nimsamehe asubuhi ya leo, nami kweli nikamsamehe katika Jina la Yesu.”]

⁵⁸ Amina. Asante, Ndugu Ben Bryant. Sasa, hiyo ni—hiyo ni kweli kabisa...nina furaha ulisema hivyo, Ndugu Ben. Mnaona, kwa kuwa watu hao wamekuwa kila mahali wakifanya marekebisho. Sasa, huo ni Ukristo halisi. Huo ni Ukristo katika matendo. Ukiwa makosani, nenda ukakubali umekosea. Unaona? Simama na useme, “Nimekosea, unaona, nisamehe.”

⁵⁹ Sasa, jamaa anayejaribu kulificha, basi yuna kitu ambacho anafunika. La, bwana, ninapenda...Kama vile maskini daktari mmoja hapa ambaye...Mnaona, hawezi...Yeye...Sitalisema juu yake, bali, kwa vyovyote vile, yeye alikuwa na kitu kidogo alichotaka kufanya, mwajua. Nami nikasema, “Loo, la, Dak, huwezi kumhonga Mungu.” Nikasema, “Inakupasa kuliweka hapa moja kwa moja juu ya ubao.” Hiyo ni kweli, uache lishuke moja kwa moja namna hiyo. Hakika, mtu huyo alikuwa kabisa hana hatia ya kujaribu kufanya jambo lolote baya. Yeye alininii tu—alidhani tu ingekuwa ni njia nzuri ambayo angeweza kujinunulia kipande cha ardhi. Wala hakuwa akitaka kulifanya vibaya, alikuwa akijaribu kulifanya vizuri. Lakini alitaka tu...Yeye alisema, “Mimi...” Alijua njia fulani angaliweza kuzungukia, ampate mtu fulani kufanya jambo fulani ambalo lingemfanya jamaa huyu kushawishika mahali hapa. Hulifanyi jinsi hiyo. Unajitokeza tu moja kwa moja. Unaona? Dumu moja kwa moja na Neno, ndipo umelipata. Dumu moja kwa moja na Neno! Mungu alimbariki na kumfanyia jambo kubwa sana. Naam, bwana.

⁶⁰ Vema, na tuviinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi. Ni wangepi wangetaka kukumbukwa katika maombi?

Ninamjua mama mmoja anayeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu bila shaka angetaka kukumbukwa, natumaini. Naye dada huyu hapa, wote, angalieni kote mahali hapa. Sasa, na tuweke kando kila kitu sasa na tuingie katika kuabudu. Hiyo ndiyo sababu tuko hapa, kwa yapata dakika zingine thelathini na tano, arobaini, kwa ajili ya ibada.

⁶¹ Sasa, Bwana, wakati tukijituliza mbele Zako, tukijisikia kwamba Yoshua wetu mkuu, Roho Mtakatifu, Kiongozi wetu wa Kiungu wa siku hizi...kama vile Yoshua alivyowatuliza hao watu mbele za Musa na kusema, “Tunaweza hata na zaidi kuiteka hiyo nchi.” Kwa sababu yeye alikuwa akiangalia, sio wale Waamaleki ama Waamori, bali alikuwa akiangalia ahadi ya Kiungu ambayo ilikuwa imetolewa na Mungu.

⁶² Na katika siku hizi za msukosuko na hali hii ulimwengu uliyomo, na juu ya asubuhi hii nzuri ya sabato, tunajituliza mbele Yako, na kusema miongoni mwa uigaji wote, kujilinganisha kwa kimwili, mbele za pepo zote waovu na walioongozwa vibaya, jinsi tunavyoliangalia Neno la Mungu na kusema sisi ni zaidi ya washindi! Mungu alisema ya kwamba Yeye atakuwa na Kanisa ambalo halitakuwa na waa wala kunyanzi ndani Yake, nasi tunajua ya kwamba tutalionga Kanisa hilo siku moja. Nasi tunajitahidi kama washiriki, tukiamini ya kwamba sisi ni washiriki wa kusanyiko hili kuu la Mungu lililozaliwa mara ya pili nalo Kanisa juu ya uso wa dunia siku hizi, tunamkaribia Mungu kwa uchaji katika Jina la Bwana Yesu.

⁶³ Nasi tunapokuja kwa unyenyekevu, tunaomba ya kwamba Wewe utaondolea mbali kutoka niani na mioyoni mwetu mambo yote ya ulimwengu, masumbuko yote ya maisha na mahangaiko, na kwamba Wewe, Ee Mungu, utatuweka katika hali ya ibada, tupate kukuabudu Wewe kwa kulisikiliza Neno Lako.

⁶⁴ Sasa, kama vile Yohana, katika somo letu asubuhi ya leo, alivyolia sana kwa kuwa hapakuwapo na mtu aliyestahili kukichukua kile Kitabu, na ndani ya mioyo yetu tungeweza kulia asubuhi ya leo, Bwana, kwa kuwa hakuna mtu anayestahili kukifungua Kitabu hiki. Bali kwa kuwa kilio cha Yohana kilikuwa ni cha kipindi kidogo tu, baadaye kidogo alifarijiwa naye Mwana-kondoo akaja na kukitwaa kile Kitabu; Ee Mwana-kondoo wa Mungu, asubuhi ya leo, njoo ukakitwae kile Kitabu na kukifungua kwetu, Bwana. Tunakungojea Wewe. Katika kupungukiwa kwetu tunangojea...Tutosheleze kwa Uwepo Wako na Neno Lako.

⁶⁵ Mikono mingi iliinuliwa Kwako, Ee Mwana-kondoo wa Mungu. Tunajua ya kwamba Wewe unaujua kila moyo, kwa kuwa Wewe ulijua makusudi yao. Nawe ungali ni Mungu leo kadiri ulivyowahi kuwa. Na Wewe daima utakuwa yeye yule, kwa sababu Wewe ni mkamilifu na asiye na kikomo wala huwezi

kubadilika. Nasi tunaomba asubuhi ya leo ya kwamba Wewe utatutosheleza, haja ya kila mtu. Tujalie, Bwana, kwamba wote wataridhika wanapoondoka humu jengoni, kwamba wamekuwa Mbele za Mungu na wanaondoka wakiwa na shauku mioyoni mwao. Bwana, usisahau kunijumuisha katika idadi hiyo, pia. Kwa kuwa naomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁶⁶ Sasa, hebu tufungue Kitabu chetu cha neema, tukimtarajia Mwana-kondoo kutufungulia ile mihuri, ama kutufungulia kile Kitabu. Hebu tufungue sasa, tuko kwenye mlango wa 5 wa Kitabu cha *Ufunuo wa Yesu Kristo*.

⁶⁷ Sasa, na kwa marafiki zangu kote katika sehemu mbalimbali za ulimwengu watakaokuwa wakisikiliza huu kupitia kwenye kanda ya sumaku, hapa ndani huenda nikasema ya kwamba sina budi kuyaelezea mafundisho na kadhalika kulifanya hili. Na mtu yeyote asiye na fundisho hana huduma. Kwa hiyo kama huwazii kwamba kusanyiko lako linapaswa kuisikiliza kanda hii, basi iweke mbali nao. Lakini ninayaelezea tu maoni yangu mwenyewe na hisia zangu mwenyewe, ufunuo wangu mwenyewe wa Neno la Mungu.

⁶⁸ Sasa, miezi michache iliyopita tulirejea nyuma na kuwekea msingi. . . siku chache zilizopita, hasa, tulirudi nyuma tukauwekea msingi mlango wa 4, mlango wa 3 hadi wa 4. Na sasa, Jumapili iliyopita, tuliwekea msingi mlango wa 4 hadi wa 5. Na sasa, leo hii, tunataka kuwekea msingi wa 5 na kuweka msingi kwa wa 6 unaokuja.

⁶⁹ Na leo hii ninakusudia kuweka Maandiko katika utaratibu, kwa kuwa labda katika siku za usoni, sijui itakuwa ni lini, lakini Mungu akitujalia, siku moja kuchukua mkutano wa siku saba humu maskanini juu ya *Mihuri Saba*. Tulikuwa na Nyakati Saba Za Kanisa, sasa tutachukua siku saba usiku juu ya ile mihuri saba ya kisiri ya Mungu, tukifungua muhuri mmoja kila usiku mpaka tuifikie hiyo Mihuri Saba. Sasa, sijui wakati Bwana atakapotupatia hilo, bali, akifanya hivyo, nitaweka tu msingi wake asubuhi ya leo.

⁷⁰ Na tukifikia kwenye vifungu vya mwisho vya maandi- . . . sehemu hapa juu, ama sehemu ya Maandiko, tutayaingiza *Yale Majuma Sabini ya Danieli*. Ndipo majuma matatu ya mwisho, tuyaunganishe na ile Yubile ya Pentekoste inayowaingiza watu kwenye mwi- . . . ile muhuri ya mwisho, kisha tukae tayari kwa ajili ya Mwana-kondoo kuifungua hiyo mihuri.

⁷¹ Basi, kumbukeni, hii mihuri ni kitu cha kisiri. Hicho Kitabu kilitiwa muhuri na ilikuwa nyuma, kilikuwa na mihuri saba ambayo hata haikufunuliwa kwenye hicho Kitabu. Mambo haya hata hayajaandikwa katika Biblia. Lakini, kama mtu yeyote angetoa tafsiri yake, ingebidi ilingane na Biblia nzima. Na, loo, nina hakika mtapata baraka kutoka kwake, ama nadhani mtaipata. Ninatumaini mtaipata.

⁷² Nilivaa koti langu kwa shida tu kwenye wakati ufaao kushuka hapa chini kwenye nuru hii ya asubuhi, kwa sababu ilikuwa... Nilikuwa nimeketi mle ndani, nikisoma, naye Roho Mtakatifu alikuwa akinibubujikia tu zaidi na zaidi kwa wema Wake. Nami... Nilipoliona jambo hilo, nikawaza, "Loo, laiti ningaliweza kulisema kule chini jinsi Wewe unavyonipa hilo hapa, sote tungekuwa na wakati mzuri sana." Lakini, kwa njia fulani, unapofika mbele za watu, basi hujisikii kama unavyojisikia wakati ukiwa peke yako katika maombi, ama chochote kingine.

⁷³ Lakini, sasa, tukianza kwenye vifungu vya kwanza, tunaona... Sasa, kuweka msingi mahali tulipoachia Jumapili iliyopita, tunaona hapa ndani ya kwamba Paulo, huko katika Waefeso 1:13 na 14, alitwambia ya kwamba sisi ni... tuna arabuni ya wokovu wetu, arabuni ya ukombozi wetu. Kwa kuwa Roho Mtakatifu ndiye arabuni ya ukombozi wetu. Na hili... Majuma machache yajayo ya mafundisho yote yatawekewa msingi juu ya ukombozi, mnaona, juu ya ukombozi, sio juu ya kuhesabiwa haki. La... Yamewekewa msingi juu ya ukombozi; sio juu ya o—ofisi ya upatanishi wa maombezi, bali juu ya *waliokombolewa*. Loo, urithi uliopotezwa ama kuachiliwa nao umekombolewa ukarejeshwa kwetu tena, na jinsi hayo yote yanavyotukia na jinsi Mungu alivyoyapanga kabla ya ulimwengu kuwapo, na jinsi Kanisa lilivyotiwa nanga salama.

⁷⁴ Nafikiri umefika wakati ambapo hatuna budi kujua jinsi tunavyosimama. Unawezaje kufanya lolote isipokuwa uwe na imani katika yale ufanyayo? Inakubidi kuwa na imani. Basi hilo ndilo kusudi langu la kufanya hivi pamoja na kanisa hapa, ni kuwapa waaminio imani na matumaini katika yale wanayotetea, kwa sababu ni Neno la Bwana. Halafu basi almuradi kote katika Maandiko limewekwa kwa ukamilifu tangu Mwanzo hadi Ufunuo, mbele na nyuma, na juu chini, hakuna njia kwa ibilisi kuingia mle mahali popote, ndipo una matumaini makamilifu, unaona, unajua mahali unaposimama.

⁷⁵ Jambo lile lile lingekuwa pamoja na dada yetu hapa aliye kwenye kiti cha magurudumu, ama labda wengine walio wagonjwa na wanaoteseka. Iwapo unaweza kuwa na ufahamu mkamilifu ya kwamba "ni mapenzi mema ya Mungu kukuponya," hakuna pepo wa kutosha nchini kukuweka ukiwa mgonjwa. Unaona? Hiyo ni kweli, unapofahamu ya kwamba ni mapenzi mema ya Mungu kukuponya, ya kwamba Yeye amelifanya kwa ajili yako, ndipo unafahamu basi jinsi ambavyo unapaswa kuenda kufanya jambo fulani.

⁷⁶ Liko hivi. Kama nilikwambia kwa moyo wangu wote... Kama ulikuwa na njaa na unakufa kwa njaa, nawe ulikuwa na matumaini makubwa kabisa kwangu kama mtu mwaminifu, nami nilikwambia ambapo dola elfu moja zilikuwa zimewekwa, jinsi ambavyo ungezipata, njia utakayopitia, mahali hasa pa

kwenda, nawe uelewe mahali hasa hizo pesa zilipo. Unaona? Basi ungeanza kushangilia papo hapo, kama tu vile ungalikuwa na hizo pesa, iwapo unaniamini.

⁷⁷ Kwa hiyo, mnaona, kabla hujapata . . . kusikia tofauti yoyote au chochote kingine, unaweza tu kuufurahia uponyaji wako katika kusema “umeupata,” kwa sababu una hakika umeupata, kwa sababu una matumaini katika Yeye aliyekuahidia huo. Mnaona? Mnaona? Ma—matumaini yako ni kwamba Yeye hawezi kusema uongo, na Yeye amekwambia mahali hasa ulipokuwa, na halafu u—una matumaini ya kwamba unaenda, unao tayari, kwa sababu hiyo ni imani yako ambayo ni arabuni ya ukombozi wako.

⁷⁸ Kwa maneno mengine, unajaribu kukombolewa kutoka kwenye maradhi, nayo imani yako ni ile bayana ya ile iliyobarikiwa . . . ama, hasa, ni arabuni ya uponyaji wako. Mradi tu kitu fulani kinasema moyoni mwako, “Mimi ni Bwana ninayekuponya *wewe*,” hilo ni zuri kutosha, hilo tu ndilo unalohitaji. Hiyo ni kusema . . . Loo, unaweza kuanza kwa furaha tu, haijalishi ni nini inatendeka. Usipoupata, hali yako ikiwa mbaya zaidi, ungali una furaha tu jinsi ulivyokuwa, ulikuwa mzima kabisa, kwa sababu unalo hakikisho hilo kwamba imekwisha. Ni wangapi wanafahamu hilo sasa, hebu tuuone mkono wako. Haya basi. “Ni ushahidi wa mambo yasiyoonekana.”

⁷⁹ Sasa, tunaona basi ya kwamba huku mwanzoni mwa huu mlango, kwamba tunaona ya kwamba wa kwa- . . . mlango wa 5 ni sehemu kubwa tu ya kuunganisha, ni—ni ki—kifungio cha almasi kinachoiunganisha sehemu ya mwisho ya wakati wa Kanisa, wa mlango wa 3. Mlango wa 4 unasimulia jinsi Yohana alivyotwaliwa Mbinguni. Nao mlango wa 5 ni utayarisho wa hii . . . Ambapo mlipitia zile Nyakati Saba za Kanisa, kisha Yohana akatwaliwa juu katika mlango wa 4. Nao mlango wa 5, yeye anaweka tu mandhari hapa kwa ajili ya kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba. Kama tu vile alivyofanya katika mlango wa kwanza wa Ufunuo, akiifungua njia kwa ajili ya zile Nyakati Saba za Kanisa (Huyo hapo amesimama kwenye vile vinara vya taa saba vya dhahabu, na Yeye anaonekana kama jiwe la Yaspi na Akiki), Naye anajiandaa kwa ajili ya zile Nyakati Saba Za Kanisa.

⁸⁰ Sasa Yeye anajiandaa kwa ajili ya kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba ya ukombozi. Mnaona, hivyo ndivyo huo mlango wa 5 ulivyo. Hiyo ndiyo sababu kidogo niliusoma kisha nikauchukua tu kutoka hapo, na kuzungumza juu yake na kutoa sehemu hizo zingine za Maandiko; ni kwa sababu sio kifungu kwa kifungu, jambo linalotukia, ni kule kujiandaa kwa ajili ya jambo fulani kutukia. Basi ukiyapata hayo maandalizi, basi unaninii tu . . . uko tayari kwa ajili yake basi. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa imani ama chochote kingine. Sasa, hili, hii mihuri . . .

⁸¹ Ninayo Maandiko fulani na maoni na kadhalika yaliyoandikwa hapa chini. Sasa, katika Waefeso 1:13-14, sisi... kama mlitaka kuliandika, kwamba, “Tunayo sasa arabuni. Roho Mtakatifu ndiye arabuni ya urithi wetu.” Kwa maneno mengine, Yeye ni hakikisho, *arabuni* ni “hakikisho,” yale “malipo ya kwanza,” ya kwamba tumepokelewa katika Kristo. Ni tumaini lililobarikiwa na kinga ya kwamba sisi tunao Uzima wa Milele na ni warithi wa kila kitu ambacho Yeye alitununulia. Loo, jamani! Mnaweza kuliona?

⁸² Loo, wakati tumetiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu (ninaendelea kulinukuu kwa maana sitaki mlikose), ni muhuri wa kibali cha Mungu kwamba kila kitu alichokifia Kristo ni mali yetu. Ni Mungu akisema, “Nimekupokea sasa, nami nitakupa Muhuri huu ya kwamba unaungojea tu wakati ule,” kwa ukombozi wetu mkamilifu, na hiyo ni kwamba tumekombolewa kwa sehemu.

⁸³ Kama nilivyosema hivi majuzi Jumapili, ninaamini ndiyo, hapa *chini* kwenye mstari huu wa chini ndipo mwenye dhambi hupitia kwenye: taka, uchafu, kinyaa, masizi. Sasa, yeye... huenda wakawa safi kama... waoe mwili kila baada ya saa nne, wanaweza wakavalia nguo zilizo bora sana, huenda wakawa ni wanachuoni hodari sana; na wenye kinyaa na wachafu kama kuta za kuzimu zenye madoa ya masizi, nafsini mwao. Mnaona?

⁸⁴ Sasa, Mkristo anaendesha juu ya hayo, kwa sababu anayo arabuni ya urithi wetu *hapa* juu. Yeye amechukuliwa, akainuliwa kutoka kwenye masizi na kinyaa; *hapa* juu, naye anaendesha juu yake. Loo, ninapenda hilo! Kama Paul Rader alivyosema wakati ule juu ya lile gogo, mwajua, yeye alisema, “Ninaendesha juu yake! Ninaendesha tu juu yake!” Hapo ndipo ilipo sasa:

Hakikisho lililobarikiwa, Yesu ni wangu!
Loo, ni maskini limbuko la jinsi gani
(nimeruhusiwa kuonja kidogo kwenye ile
Chemchemi.) ya utukufu wa Kiungu!
Mimi sasa ni mrithi wa wokovu, nimenunuliwa
na Mungu,
Nimezaliwa kwa Roho Yake na kuoshwa kwa
Damu Yake.

Si ajabu hii ndiyo hadithi yangu, huu ndio
wimbo wangu,
Kuimba—kuimba sifa Zake siku nzima.

⁸⁵ Mnaona, nimeinuliwa juu ya vivuli, kutoka kwenye masizi, limbuko! Tunayo arabuni sasa ya urithi wetu mkamilifu, kwa sababu Mungu tayari ameing'oa mizizi ya ardhini kutoka kwenye mambo ya ulimwengu na ametupanda kwenye ardhi za juu zaidi; akaniinua juu, akaniweka vema, akanibadilisha kutoka kwenye mambo ya ulimwengu; akaing'oa mizizi, matawi,

kila kitu, kisha akaniinua juu, kutoka kwenye udongo wa kinamasi, kutoka kwenye taka za kale za dhambi; akanipanda juu ya Mlima Sayuni, nimeketi kwenye bustani ya wapendwa, Watakatifu wa Mungu. Na sasa sisi ni wenyeji wa Ufalme huo, ndugu na dada katika Kristo Yesu, takataka zote na uchafu na chuki yote vimetoka niani mwetu. Maji yetu . . . miili imeoshwa kwa maji safi na mioyo yetu imenyunyiziwa Damu ya Bwana Yesu, naye Roho Mtakatifu anakaa pamoja na upepo Wake mwanana unaovuma kupitia kwenye matawi siku nzima, akitutikisa na kutusukuma na kutufanya tushike mizizi vizuri na kukulia chini kilindini. Hilo si ni zuri sana? “Arabuni ya wokovu wetu.”

⁸⁶ Urithi wetu uliopotea, mlango huu unaufunua. Urithi wetu uliopotea umerejeshwa na Mkombozi wetu wa thamani wa Jamaa wa karibu. Jinsi Mungu alivyoshuka na kufanyika . . . akabadilisha umbo lake kutoka kwa Mungu na akafanyika mwanadamu, kusudi aweze kuwa mwanadamu, apate kuwa Mkombozi wa Jamaa wa karibu wa wanadamu, aukomboe ulimwengu wa kawaida uwarudie watu wa kawaida. Amina! Jinsi ambavyo Mungu (wa Kimbinguni) alivyofanyika wa kawaida apate kuwa wa Jamaa wa karibu, kwa sababu asingeweza kuasi sheria Zake Mwenyewe. Ilibidi aje kwa u- . . . ukombozi wa jamaa wa karibu kwa kuwa hivyo ndivyo Yeye . . . huo ndio mpango Wake. Hivyo ndivyo Yeye alivyolifanya.

⁸⁷ Mungu akijua ya kwamba mwanadamu angeanguka, hata hivyo Yeye hangeweza kumfanya mwanadamu aanguke. Mungu akijua ya kwamba mwanadamu angepotea, ingawa Yeye hakutaka yeyote apotee. Lakini kusudi yale madhihirisho makuu ya sifa za Mungu yaweze kudhihirishwa kwa wanadamu wote, ya kwamba Yeye angeweza kuwa Mkombozi, Yeye angeweza kuwa Mwokozi, ilibidi mwanadamu aanguke. Ilikuwa ndani yake kuanguka, ndipo ilikuwa ndani ya Mungu kumkomboa tena. Hiyo ni u- . . . hatuna budi kuwa na usiku, kuufanya mchana kuwa sahihi. Hatuna budi kuwa na maradhi, kutufanya kuifurahia afya. Kila kitu, kibaya na kizuri. Sasa, naye Mkombozi wetu wa Jaama wa karibu . . .

⁸⁸ Sasa, ninawatakeni muone hapa. Ninaangalia moja kwa moja hapa kwenye mlango huu wa 5, wakati alipoiangalia, “Usiogope!” Katika kifungu hiki cha 5, “Usiogope!” Mnaona, daima kuna . . . Hutaki kuhofia chochote.

. . . mmojawapo wa wale wazee akaniambia, Usilie: tazama, Simba wa kabila la Yuda, Shina la Daudi, yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu, na zile muhuri zake saba.

. . . kisha, nikaona, tazama, katika . . . tazama, katikati ya kile kiti cha enzi na . . . wale wenye uhai wanne, . . . katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama . . .

89 “Mwana-kondoo.” Kwa nini yeye hakumwona huyo Mwana-kondoo hapo awali? Huyo Mwana-kondoo alikuwa ameketi juu ya Kiti cha Enzi cha Baba, ndani ya wale—wale walinzi. Yohana asingeweza kuona mle ndani, yeye aliwaona tu hao wenye vichwa vinne...ama wale wenye uhai wanne wamesimama pale, ama wale Makerubi wanne wamesimama pale wakilinda Mahali hapo Patakatifu. Nasi tulilipata Jumapili iliyopita, na katika masomo hayo mengine, ya kwamba aliwaona hao bali asingeweza kuona kilichokuwa mbele ya hao. Na mle ndani, mara ghafla, kukatokea...kisiri tu, mara moja, akatokea Mmoja, Mwana-kondoo.

90 Sasa, kuonyesha hakuwa ni mnyama wa kawaida, mwana-kondoo, kwa sababu Yeye alikitwaa kile Kitabu kutoka mkono wa kuume wake Yeye aliyeketi kwenye Kiti cha Enzi; mwana-kondoo asingeweza kufanya hilo, mnaona. Yeye alikuwa—Yeye alikuwa—Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo, alikuwa ni Kristo. Kwa maneno mengine, katika sifa Zake Yeye alikuwa ni mpole na mnyenyekevu kama mwana-kondoo.

91 Sasa, angalieni, ilikuwa ni Mwana-kondoo Mkombozi, Mwana-kondoo Mkombozi kama tu yule wa kwanza. Mungu kamwe hawezi kubadilika! Amina! Mkombozi wa kwanza alikuwa ni mwana-kondoo, katika bustani ya Edeni, alikuwa ni mwana-kondoo ambaye Mungu alimtoa. Basi huyu hapa tena, moja kwa moja katika Ufunuo, ni Mwana-kondoo tena. Kukomboa nini? Hali ya kuanguka na urithi ulioanguka wa jamii ya watu walioanguka. Mwana-kondoo anarudi kukomboa, kama vile wetu alivyokuwa hapo mwanzo, kutukomboa.

92 Kukomboa kitu gani? Atatukomboa kwa nini? Kuvunja... kuileta kwenye...Chochote kinachokombolewa ni kile kimepotea. Ni kitu kilichokuwa kimepotea na halafu kimerejeshwa tena. Anaturudishia nini, Mwana-kondoo huyu? Kila kitu tulichokuwa nacho hapo mwanzo.

93 Tulikuwa na nini hapo mwanzo? Uzima wa Milele. Tulikuwa ni warithi wa ulimwengu. Tulikuwa na Uzima, haikutubidi kufa. Haikutubidi kuwa wagonjwa. Haikutubidi kuzeeka. Hatukuwa na hofu zozote. Ambako hakuna mazishi, hakuna makaburi, hakuna uovu, hakuna mauti, hakuna nywele zenye mvi, hakuna mabega yaliyoinama, hakuna maombolezo, hakuna kulia. Tulikuwa na Uzima, wa Milele! Tulikuwa na mamlaka juu ya dunia yote. Tulikuwa tu ni mungu (hivyo tu) duniani; tunatembea-tembea, na kama mti huu haukuonekana vema kusimama hapa, tungenema, “Ng’oka ukakae hapa,” nao ungefanya hivyo. Upepo ulikuwa ukivuma, hatukutaka upepo uvume, “Amani, tulia,” nao ukatulia. Na Yeye alikuja kufanya nini? Kuyakomboa hayo yote aturejeshee tena (Loo, loo, loo, loo, loo, jamani!), kurejesha hayo yote tena.

⁹⁴ Na sasa maumbile yenyewe yanaugua, yakingojea nini? Kudhihirishwa kwa wana wa Mungu, wana wa Mungu wapate kudhihirishwa.

⁹⁵ Nasi tuna arabuni ya wokovu wetu sasa, na tunaweza kumchukua ndugu yetu anayekufa kwa kansa, na kusimama tukiwa na maskini pumzi hiyo ya ukombozi, na kuomba maombi ya imani juu yake ambayo yatakibadilisha kivuli hicho cha mwanadamu kiwe mtu mwenye afya tena; tutafanya nini wakati umilikaji wetu mkamilifu utakapokuja? Amina!

⁹⁶ Maumbile yanajua hilo. Maumbile yanaugua nasi tunaugua pamoja nayo. Maumbile yanangojea kule kudhihirishwa kwa wana wa Mungu, kwa sababu maumbile yalilaaniwa pamoja na bwana wake. Wakati bwana wake alipolaaniwa (aliye juu sana), basi maumbile yalianguka pamoja na bwana wake. Lakini wakati Mkombozi huyu wa Jamaa wa karibu alipokuja (Haleluya!) na kumkomboa mtu ambaye ni mtawala wa maumbile. Basi maumbile yote yanamngojea huyo mwanadamu, bwana wake.

⁹⁷ Tunafanya nini? Tunachukua shoka na kulishika mikononi mwetu na kuukata mti tukitaka; lakini siku hiyo hatutafanya hivyo. Amina!

⁹⁸ Maumbile yote yanamngojea bwana wake. Naye huyo bwana ni wana wa Mungu waliopewa dunia hii. Sasa, Mungu atakuwa na mbingu Zake, hakika, bali hii ilipewa mwanadamu. Naye Mkombozi wa Jamaa wa karibu akaja kutukomboa aturejeshe kwenye yale tuliypoteza. Ni jambo zuri jinsi gani! Jamani! Ninafikiri tu hiyo ni . . . “Mwana-Kondoo Mkombozi.”

⁹⁹ Wakati kazi itakapomalizika, tutakuwa na vitu vyote tena. Vitu vyote vya aina gani? Tuna nguvu zote. Tunao Uzima wa Milele. Tunayo afya ya Milele. Tunao ujana wa Milele. Tunazo nguvu za Milele. Loo, sisi ni wa Milele tu pamoja na wa Milele! Halafu, basi, sisi sote tunaungojea wakati huo uje, tuingojea na kuugua, tuingojea.

¹⁰⁰ Nacho Kitabu hiki cha sehemu saba cha mipango saba ya ukombozi kimeletwa kwetu, na hayo ndiyo Kitabu hiki kinayoshikilia. Sasa, tutaenda kwenye mlango wa 10 ambapo Malaika huyu mwenye nguvu anatangaza kitu fulani ambacho . . . na Yeye alikuwa na Kitabu kidogo ambacho ilimbidi Yohana kukila. Ndipo alipofanya hivyo, akakiingiza tumboni mwake nacho kilikuwa ni kichungu, bali midomoni mwake kilikuwa ni kitamu.

¹⁰¹ Inapokulazimu kukimeng’anya, basi kinakuwa ni kichungu, kila mtu anakupinga, kila mtu akikwambia “Wewe ni mtakatifu anayejibingirisha, wewe ni *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*.” Unaona? “Ume—ume—umerukwa na akili zako.” Kwa hiyo ni vigumu kukimeng’anya; bali unapoushuhudia Utukufu Wake, ni kitamu midomoni mwako. Hivyo tu. Unaona? Na wakati unaposimama

mkutanoni, unasema, “Utukufu kwa Mungu! Hale-...” Loo, unapopitia kwenye huo mzingiro mkubwa, ni vigumu; lakini basi unapotoka kwenye huo mzingiro mkubwa unaweza kushuhudia habari zake, ndipo ni kitamu midomoni mwako. Unaona? Hiyo ni kweli. Hicho ni Kitabu hiki cha ukombozi.

¹⁰² Sasa, sasa, tunataka kutoa mfano mwingine mmoja mdogo katika kifungu cha 5 hapa, ndipo tutaanza kwenye... tutachukua kifungu chetu cha 6 na kuanza. Sasa, ninawatakeni muone katika ule mpango wa ukombozi jinsi ambavyo Mungu alitangulia kulionyesha, Yeye alilishughulikia kikamilifu katika Ruthu na Boazi. Mimi... Hapo ndipo tulipoishia Jumapili iliyopita. Sasa, ninataka kuanzia papo hapo sasa, leo hii, juu ya Ruthu na Boazi.

¹⁰³ Sasa, kuna vituo vinne, ama, njia panda nne katika Ruthu na Boazi. Ya kwanza ni Ruthu *akiamua*. Ni wangapi wamewahi kusikia ninii... mimi nikiuhubiri ujumbe huo? Hebu tuone mikono yenu. Ninajua... Vema, ninyi nyote, nadhani. Nimeuhubiri hapa, na nimekuwa nao kwenye kanda na kadhalika. Ruthu, kwanza, ilimbidi *kuamua* kama ataenda kwenye nchi hii, ama la, pamoja na Naomi. Ilimbidi *kuamua*. Ndipo baada ya kufika huko, jambo la pili lililimbidi kufanya lilikuwa ni *kutumika* shambani mwa Boazi; huko nje, miguu mitupu, akiokota masazo nyuma ya wale wavunaji, akitumika. Ndipo akiisha kupata neema machoni pa Boazi, basi ilimbidi *kungojea* mpaka Boazi alipofanya kazi ya ukombozi wa jamaa wa karibu, apate kurejesha yote ambayo Naomi alipoteza ili aweze kumleta Ruthu ndani, yule Mumoabu. Halafu basi hatua inayofuata, ni—ni Ruthu *akizawadiwa*.

Sasa, angalieni. Ruthu, *akiamua*, kikamilifu...

¹⁰⁴ Loo, mtu yeyote asemaye “hiyo Biblia haikuvuviwa,” hao wana kasoro fulani. Kila Neno Lake limevuviwa, kila Neno Lake huunganika pamoja kama tu kuumana kwenye—kwenye—kwenye ubao. Linaendana tu kikamilifu kama vile meno kwenye gurudumu kubwa mno linalozunguka, limepimiwa tu wakati kufikia sehemu moja katika milioni ya sekunde, kamilifu tu kabisa.

¹⁰⁵ Sasa, angalieni katika hili sasa, Ruthu, *akiamua*, ilimbidi kufanya uamuzi kama ataamua kwenda kule ama la. Ilimbidi *kuamua*. Sasa, hivyo ndivyo kila mwaminio hana budi kufanya. Huna budi kuyaacha matembezi yako ya kale, huna budi kuyaacha maisha yako ya kale, huna budi kuacha mambo ya ka—kale ya ulimwengu.

¹⁰⁶ Ndugu Roy, Dada Roberson alishikwa na ugonjwa? Loo, nilidhani labda alikuwa mgonjwa ama kitu fulani. Nilikuwa nikitaka kusema aletwe hapa juu endapo alikuwa ameshikwa na ugonjwa ama kitu fulani.

107 Iliwabidi kuyaacha matembezi ya kale ya maisha, ama kitu kama hicho, na—na wavuke waingie katika nchi mpya, pamoja na watu wapya ambao kamwe hukuwajua hapo awali. Hivyo ndivyo ulivyofanya, hapo ulipofanyika Mkristo? Uliacha nyumba ya biliadi, uliacha vilabu vya usiku. Ilibidi uingie kwenye kundi la watu walioonekana kana kwamba walikuwa na mitukutiko, walishtuka-shtuka na kutetemeka na kulia, na kutikisa kichwa chao na kurukaruka, na, mbona—mbona, lilikuwa ni—lilikuwa ni—ni—ni “kundi la wendawazimu” kwako. Kwa hiyo ilibidi ufanye uamuzi kama utaenda ama hutaenda. Hiyo ni kweli. Nawe ulijua ya kwamba ulipofanya hilo, watu wako mwenyewe walikuwa wanaenda kukudhihaki, wale uliokuwa umewaacha. Hiyo ni kweli? Hiyo ni wazi tu. Unaninii tu... wanapaswa kutarajia hilo kwa kuanzia, maana hivyo ndivyo ilivyo.

108 Sasa, Ruthu alikuwa na jambo lile lile. Wamoabu wangemwambia nini wakati alipovuka kuenda Israeli, kwa kundi la walokole? Mnaona, ilimbidi kufanya uamuzi. Ilimbidi kuamua. Nawe inakubidi kuamua. Basi, hatimaye, hapo alipofanya uamuzi wake, alienda huko kwenye n—nchi mpya.

109 Sasa, huko ni kuhesabiwa haki. Je, hiyo ni kweli? Sasa, liangalieni Kanisa hili. Loo, ni kamilifu.

110 Mnajua jinsi sisi... Ni wangapi wenu waliousikia *Uzao wa Ibrahimu* wakati nilipohubiri juu ya hilo? Jinsi ambavyo *kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo* wa Roho Mtakatifu. Sasa, angalieni kama hili ni kweli ama la.

111 Ruthu, akifanya *uamuzi* wake, mfano wa Kanisa, Kanisa la Mataifa. Yeye aliamua, kisha akavuka akaingia katika hiyo nchi. Sasa, mara nyingi, sisi Wamethodisti na Wabaptisti, tunafikiri hayo ndiyo yote yakupasayo kufanya. Yeye alikuwa tu ameanza! Hakuwa amefika popote bado, aliingia tu nchini.

112 Sasa, jambo lingine lililombidi kufanya, ilimbidi *kufanya kazi*. Akawa mshika sheria. Ilimbidi “kuutimiza wokovu wake mwenyewe kwa kuogopa na kutetemeka” kama wewe ulivyofanya. Alitoka akaenda shambani na kuweka nguo zake juu yake, akaingia shambani na kuokota masazo nyuma ya wasichana kusudi apate riziki ya hiyo siku. Hiyo ni kweli? Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akijaribu kupata kibali cha Boazi. Kwa hiyo akafanya kazi kupitia ile hatua ya ushika sheria.

113 Na hivyo ndivyo Kanisa lilivyofanya hasa. Walutheri waliliamini kwa imani nao wakaingia nchini. Lakini Methodisti ilifundisha utakaso, ambao ulikuwa ni msimamo Wake wa kisheria, mnaona, “Huna budi kufanya jambo fulani.” “Sina budi kuacha! Sina budi kuacha nywele zangu zikue,” walisema wanawake. Hakika, hawafanyi hivyo tena; bali kweli wa—walifanya hivyo, waliacha nywele zao zikue. Iliwabidi kuacha

kujipaka rangi nyusoni mwao. Hawakuva sketi za—zao vibaya na—na, ama, kaptura kama hao wengine walivyofanya. Iliwabidi kufanya jambo fulani. Mnaona? Hivyo ndivyo yeye alivyofanya, ile hatua ya kuhesabiwa haki, ile hatua ya kutakaswa.

¹¹⁴ Sasa, wakati hatimaye alipopata kibali kwa Boazi, kulifanyika nini? Ndipo Naomi akamwambia, “Wewe *ngojea* hapa wakati Boazi anapofanya kazi ya mkombozi wa jamaa wa karibu, maana yeye ndiye pekee anayeweza kuifanya. Yeye ndiye mkombozi wa jamaa yetu wa karibu, nawe ngojea tu hapa. Usiende mashambani tena. Usifanye *hili, lile*, ama *linginelo*. Wewe ngojea tu mpaka ukombozi wa jamaa wa karibu umetimizwa.” Ndipo yeye *akapumzika*. Amina!

¹¹⁵ Hilo hasa ndilo Kanisa limefikia katika hatua hii ya mwisho ya Pentekoste. Mnaona? Mwanzoni mwa Pentekoste wote walifanya kazi nao “iliwabidi kufanya *hivi*,” nao wakawatikisa na kila kitu kingine. Sasa Kanisa linafanya nini? Kanisa la kweli *linapumzika* tu. Raha ni nini? Hili hapa, *Raha* ni “Roho Mtakatifu,” ile siku ya *Sabato*. (Wadventista Wasabato wanataka kutwambia, mwajua, kwamba ni sabato ya siku ya saba ama kitu kama hicho.) Katika Waebrania mlango wa 4, ilisema, “Sisi tulioingia katika *Raha* Yake tumepumzika kutoka kazi zetu wenyewe kama vile Mungu alivyopumzika kutoka kwa Zake.” Kwa hiyo *sabato* ni Roho Mtakatifu.

¹¹⁶ Basi wakati Ruthu alipokuwa *akipumzika*, ilikuwa ni mfano wa Kanisa likipumzika katika ahadi za Mungu! Tunayo arabuni sasa ya wokovu wetu. Hatuna wasiwasi kama tunaenda kule ama hatuendi, tunaenda! Hiyo ni kweli. Mungu alisema hivyo! Mungu aliliahidi nasi tunayo arabuni (Amina.), tayari tumepokelewa, Kristo ametukubali. Hakuna njia ya kuliondokea sasa, tupo hapo! Amina! Yote itupasayo kufanya ni kungojea tu mpaka ninii . . . Yeye achukue . . . Yeye anafanya kazi ya Mkombozi wa Jamaa wa Karibu. Tunayo arabuni yake sasa hivi, tukiungojea wakati ambapo Yeye atarudi.

Halafu basi jambo lingine alilokuwa Ruthu, Ruthu *alizawadiwa*.

¹¹⁷ Hivyo ndivyo Kanisa lilivyofanya. Lilingia katika kuhesabiwa haki, chini ya Luther. Likaingia katika utakaso, chini ya Wesley. Likaingia katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, katika siku hizi za mwisho. Na sasa *linapumzika* pamoja na arabuni ya urithi wetu ambapo tunajua kwamba jambo fulani lilitukia ndani yetu, tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, nasi tunangojea, tukiugua pamoja na maumbile, kwa ajili ya wakati huo ambapo tutapokea Uzima usiopatikana na mauti, utimilifu usiopatikana na mauti; miili yetu itakombolewa. Kila kitu kimekombolewa, nasi tunamngojea tu Yeye arudi kutoka langoni. Amina!

118 Ndipo nini? Ruthu *alizawadiwa*. Hapo ndipo tutakapozawadiwa. Hayo ndiyo Kitabu hiki kilichotiwa muhuri kwa mihuri saba kitakayotufungulia. Mambo haya ni nini? Ni siri. Hayajaandikwa katika Neno, hayana budi kufunuliwa na Roho Mtakatifu; bali kama utaangalia, kwa kweli, yamefunuliwa kote kote katika Maandiko lakini yamefichwa kutoka kwa watu. Tutakapofikia kwenye lile gombo baada ya kitambo kidogo, mtaona vile liliyopangiliwa, ndipo mtajua jinsi hayo mambo yanavyofunguka.

119 Sasa, naam, *kupumzika*. Yale Ruthu chini ya kuhesabiwa haki... Mnaliona, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ruthu chini ya utakaso, *kufanya kazi*, mshika sheria. Ruthu, *akipumzika*, akimngojea Boazi arudi kutoka kwenye kazi iliyomalizika.

120 Sasa, Boazi wetu kweli aliimaliza kazi pale Kalvari. Lakini kabla Yeye hajaja kutupeleka Nyumbani Mwake, Yeye anaenda Nyumbani kwanza (katika Yohana 14) kutuandalia mahali. Utukufu!

Msifadhaike mioyoni mwenu: kama mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.

Nyumbani mwa Baba yangu kuna makao mengi: kama haikuwa hivyo, ningaliwaambia. Lakini naenda kuwaandalia mahali.

Basi... rudi tena, ili niwakaribishe...

121 Mnaona, Boazi anashuka, yeye alifanya nini? Anashuka, anasimama... akawachukua wazee akaenda mbele ya lango, akavua kiatu chake, na kusema, "Na ijulikane leo hii ya kwamba nimemkomboa Naomi na urithi wake wote." Akamchukua yule Mmoabu pamoja nao.

122 Basi Yesu alipokuja, Yeye alikuja kumkomboa nani? Israeli. Alifanya nini katika kuwachukua Israeli? Alimpata Bibi-arusi wa Mataifa. Hakika, Yeye alimpata, hapo Yeye alipowachukua Israeli. Alienda... Na Yeye alipoenda kwa walio Wake Mwenyewe, ilimbidi kufanya hivyo. Jambo la kwanza lililimbidi Yeye kufanya lilikuwa ni lipi? Kuwakomboa walio Wake Mwenyewe. Nalo Kanisa la Mataifa ni dada tu wa mwanamke huyo, kanisa la Israeli. Bila shaka! Kwa hiyo ilimbidi kuwakomboa Israeli kusudi alipate *Hili*. Naye ilimbidi kumkomboa Naomi kusudi ampate Ruthu, bibi-arusi wake.

123 Sasa, yeye alifanya nini? Kabla hajaweza kumchukua... Loo, utukufu! Whiu! Alifanya nini? Anatoka anaenda shambani, nadhani alipaka rangi kila kitu na kuweka mazulia mapya sakafuni. Loo, hu—huenda alijenga nyumba mpya. (Kwetu sisi, ni Nyumba mpya.) Ndipo akaandaa kila kitu, kisha akarudi amevaa shada la kifua kwa ajili ya arusi. Amina!

¹²⁴ Ruthu alikuwa akifanya nini? Si hata jambo moja. Kupumzika! Kungojea! Hakuna kutenda kazi tena, hakuna masumbuko tena!

¹²⁵ “Ni lazima niwe Mmethodisti? Ni lazima nijiunge na Baptisti? Ni lazima niwe Mpresbiteri?” La, bwana, mpate tu Roho Mtakatifu kisha upumzike. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Tunakutazamia kuja kwa siku ile nzuri ya
Utawala wa Miaka Elfu, (Utukufu!)
Wakati Bwana wetu mbarikiwa atakapokuja
kumchukua Bibi-arusi Wake anayengoja;
Loo! Dunia inaugua, inalia kwa ajili ya ile siku
ya kufunguliwa kutamu.

Vyote, maumbile yanaugua, majani ya mtini, kila kitu kinaingojewa siku ile ya kufunguliwa kwenye baraka, wakati Mkombozi wa Jamaa wa Karibu atakaporudi na kumchukua Bibi-arusi Wake.

¹²⁶ Sasa Yeye anapumzika. Chini ya utakaso? La. Chini ya kuhesabiwa haki? La. Lakini chini ya *kuhesabiwa haki, utakaso*, na kuingia katika *raha* pia.

¹²⁷ Sasa, Isaya, mlango wa 28 na kifungu cha 18, inasema:

... *amri juu ya amri, ... kanuni juu ya kanuni, ...*
huku kidogo, na huku kidogo: shikilia sana yaliyo
mema.

Kwa kuwa kwa midomo migeni na kwa lugha zingine
nitasema na watu hawa.

... Na *hii ndiyo raha*, hii ndiyo sabato ... hii ni wakati
Kanisa linaingia ndani likangojee.

¹²⁸ Angalieni jinsi tumepitia moja kwa moja kwenye kuhesabiwa haki, utakaso, sasa tukaingia katika ubatizo wa Roho Mtakatifu: kupumzika, kungojea. Kitu gani? Na sasa, sasa, tunapozifikia funuo hizi mtaona jinsi ilivyo sasa. Mnaona? Jinsi ambavyo ninii tu ... Mambo haya yasingeweza kufundishwa mpaka siku hii. Hayakufundishwa, hayangeweza kufundishwa. Hayakufunguliwa kwa wana wa binadamu. Biblia ilisema hivyo. Ninaweza kuwaonyesha hapa katika Maandiko ya kwamba ilisema yasingefunguliwa mpaka (wana wa binadamu), hata siku hii. Na sasa tunayamalizia kwenye mambo haya makuu yaliyobarikiwa. Sasa ... Vema.

¹²⁹ Kifungu cha 6 ... Ama sehemu ya cha 5, yule mzee katika kifungu cha 5 alikuwa sahihi hapo aliposema, “Tazama, Mwana-kondoo!” Lakini, alipoangalia kote, alimwona Simba. Ilikuwa ni Simba badala ya Mwana-kondoo. Lakini basi ilikuwa ni kitu gani? Kazi Yake ya upatanisho ilikuwa imekamiliwa, ya upatanisho. Yeye alikuwa ... aliacha kuwa Mpatanishi mwishoni mwa wakati wa Kanisa, apate kuwa Simba wa kabila la

Yuda, kazi Yake ya upatanisho ilikamilika. Na Yeye alikuwa awe Simba ambaye alikuwa ni Hakimu, sasa, ndipo Yeye akachukua... wakati alipokitwaa kile Kitabu kutoka kwenye ule mkono.

¹³⁰ Sasa, kumbukeni, wakati mtu alipoenda kukomboa (Msisahau hili, sasa.), wakati mtu alipoenda kukomboa, aliwachukua watu pamoja naye akaenda kwenye malango ya mji, wakiwa ni wazee, na hapo a—a—akatangaza kusudi lake la kuwa pale. Hivyo ndivyo yeye alivyofanya, alienda langoni, kasema, “Niko hapa kujitangaza mwenyewe kuwa ni mkombozi wa jamaa wa karibu wa urithi huu, nami nipo hapa nikijitambulisha mbele ya wazee hawa wa mji.” Mnaona?

¹³¹ Na wakati ninii... Yohana alilia. Sasa, mtu fulani, kama nilivyosema juma lililopita, wao walisema, “Yohana alilia kwa sababu kwamba hangeweza kupata mtu yeyote aliyestahili.” Sivyo ilivyokuwa. Mtu aliye chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu asingelia kwa sababu hiyo. Aliwazia kwamba, “Maana yeye hakustahili,” labda Yohana mwenyewe hakuwa amestahili. Hakuna mtu aliyestahili. Lakini hakulia kwa sababu hiyo.

¹³² Ninaamini alikuwa akilia kwa furaha kwa sababu kwamba alikuwa ameuona mpango wote wa ukombozi ulioandikwa kwenye Kitabu hiki hapa. Haikuwa ni kwa sababu hapakuwapo na mtu aliyestahili, kwa sababu, hapo alisimama Mwana-Kondoo papo hapo aliyestahili. Kwa hiyo yeye alikuwa akilia, hapo akasema, “Loo, utukufu kwa Mungu!” Msikilizeni mara moja wakati anapoanza kupiga makelele. Sasa, bali tunamwona hapa akilia kwa sababu alikuwa na furaha kwa kuwa yule Mwana-kondoo alikuwa amekitwaa kile Kitabu kwa ajili ya... kutoka kwenye mkono Wake aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi.

¹³³ Na mara alipofanya... Wakati Malaika huyu, Malaika huyu mwenye nguvu, alipolia “Ni nani anayestahili?” yeye alikuwa akitangaza papo hapo, alikuwa akitangaza kwa ajili ya Mkombozi wa Jamaa wa karibu. Na mara baada ya hayo, yeye akasema, “Ni nani anayestahili kukitwaa Kitabu?” Ndipo kitu fulani... Ndipo Yohana akaanza kulia. Ndipo kukatokea nini? Akaona, hapo kikasimama kile Kitabu. Hicho hapo, bali ni nani aliyestahili?

¹³⁴ Vema, hapo alisimama Gabrieli, hakika, alistahili; bali, mnaona, yeye hakuwa mwanadamu, naye alikuwa ni Malaika. Pia hapo alisimama Mikaeli, alistahili; ila yeye hakuwa mwanadamu, alikuwa ni Malaika. Kwa hiyo ilibidi iwe ni mtu fulani ambaye alifanyika mtu wa duniani kama tulivyofanyika sisi. Ndipo basi wakati alipomwona Mwana-kondoo huyu aliyekuwa amechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, akija, naye akaona ya kwamba alikuwa amechinjwa kote kote

hata kuwekwa misingi ya ulimwengu, ndipo Yohana akalia. Amina! Maana hilo hapo, yeye aliona jambo hilo lote. Mnaona?

¹³⁵ Basi mara alipotangaza “Ni nani anayestahili?” alikuwa akitangaza kule kuja kwa Mkombozi wa Jamaa wa karibu. Naye huyu hapa amesimama, Mwana-kondoo. Basi alifanya nini? Akaenda kwenye Kiti cha Enzi alipokuwa Roho wa Mungu, akakitwaa kile Kitabu katoka kwenye mkono wa kuume wa Yeye aliyeketi juu ya kile Kiti cha Enzi. Nao wale wazee wote wakaanguka chini na kusema, “Wastahili kwa sababu Wewe ulichinjwa.” Mnaona? Ndipo Yeye akawa basi. . . Kitabu Chake, ama angalau Kitabu cha ukombozi, ama—ama Kitabu cha uombezi katika wakati wa Kanisa kilikwisha, sasa Yeye anakuwa Mkombozi.

¹³⁶ Sasa, kufunuliwa kwa jinsi Yeye alivyofanya hivyo kutakuwa kwenye hii Mihuri Saba. Sasa, tunaona katika ninii. . . kama vile wakati kile Kitabu cha kazi ya upatanisho Wake kilipofanyika, hiyo kazi ilipomalizika, sasa katika milango mitatu ya kwanza ya Kanisa, imekwisha. Lakini sasa ukombozi, ukombozi utafunuliwa. Ni kitu gani? Sasa, wakati Yeye alipokitwaa Kitabu hiki. . . Sasa, jaribu kujitwika mawazo yako yenye kilindi, maana, kama tukiwahi kuzipata siku hizi saba usiku, mtaninii—mtalipata sasa.

¹³⁷ Usipolipata, inua tu mkono wako, useme, “Si—silipati,” mnaona, angalieni, maana ninawatakeni muwe na uhakika sasa.

¹³⁸ Sasa, angalieni “Ukombozi.” Baada, mara baada ya uombezi Wake kumalizika kwa ajili ya Kanisa, basi Yeye anajifunua Mwenyewe kama Mkombozi wa Jamaa wa karibu. Mnalielewa hilo sasa? Na sasa Yeye anaenda kulifunulia Kanisa jinsi alivyofanya hilo. Ndipo basi ikiwa ufunuo huu umeanza tayari, basi hiyo inathibitisha ya kwamba tuko kwenye mwisho wa safari. Amina! Sasa, angalieni tu kama Hili. . . kama ni kweli ama si kweli, tunapoyapitia Maandiko haya hapa.

¹³⁹ Tunaona: Ni kitu gani kilichokuwa kikifunuliwa? Ufunuo wa ukombozi ni nini, tulikombolewaje? Angalieni tu hapa katika miaka hii michache iliyopita kile kimetukia: ule ufunuo wa Jina la Yesu katika ubatizo wa maji, ufunuo wa kutokuwako na jehanamu ya Milele, kamwe haukujulikana hapo kabla (kuwazia wapendwa wenu wangekuwa huko Milele). Mnaona?

¹⁴⁰ Wala huwezi kuwa na Uzima wa Milele isipokuwa umeokolewa. Ukiwa na Uzima wa Milele, basi huwezi kuchomwa moto katika jehanamu Milele. Utaadhibiwa kwa ajili ya dhambi zako kwa maisha yako ya kawaida, bali huwezi kuwa na Uzima wa Milele katika jehanamu. Iwapo unao Uzima wa Milele, basi huwezi kuchomwa milele kwa sababu kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Nami nina hakika Kanisa linafahamu hilo.

¹⁴¹ Sasa, ni kitu gani? Mambo gani mengine? Ule mpango wa ukombozi. Angalieni tu kile tumepewa juzijuzi na Roho Mtakatifu, mnaona: Uzao wa Ibrahimu, yale huo ufunuo uliyomaanisha.

¹⁴² Ule uzao wa nyoka. Mnakiona Kitabu hiki cha Ufunuo? Angalieni tutakapokifikia, jinsi kinavyolimenya. Nami nililithibitisha papa hapa kwa Maandiko, hiyo ni Kweli kabisa. Ninarudi moja kwa moja katika Ufu-...ama, moja kwa moja ninarejea katika Mwanzo na kulichukua na kuonyesha wakati muhuri huo ulipofunguliwa ulishuka moja kwa moja kote katika Biblia, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo.

¹⁴³ Wazieni tu, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo kamwe hapakuwapo na mtu yeyote aliyebatizwa katika jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Ni ubatizo wa uongo! Nilisimama mbele ya wahubiri mia tatu na kitu wa shirika lililo kuu zaidi la wahudumu wa Chicago hivi majuzi, na kuthibitisha hilo hata wote wakalia wenyewe kwa wenyewe. Sabini wa hao wanakuja kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu.

¹⁴⁴ Nao ule uzao wa nyoka umekuwa ni kutoka Mwanzo! Ikiwa yule nyoka hakuninii...kama hakuwa na uzao, basi Kristo hakuzaliwa; kwa sababu Yeye alisema, “Nitaweka uadui kati ya Uzao wako na uzao wa nyoka.” Basi iwapo uzao wa nyoka ulikuwa ni hadithi ya uongo vivyo hivyo na Kristo alikuwa ni hadithi ya uongo, vivyo hivyo na Kanisa ni hadithi ya uongo, unaona ni yote, huwezi kuyatenganisha. Nyoka alikuwa na uzao, na hilo ndilo linalowaduwaza kweli. Kwa nini hawawezi kulielewa? Kwa sababu hawana ufunuo wake.

¹⁴⁵ Kwa nini hawaji na kulibishania pamoja nami? Mimbara imefunguliwa wakati wote, nitakutana na mtu yeyote. Nisingebishana nao, bali hakika ningejadili hilo nao, kama wakitaka...Niliwauliza pale pale mbele ya hilo shirika. Ninataka baadhi yenu waniambie mahali limekosea! Usisimame pembeni mahali fulani na kuzungumza habari zangu, kuhusu hilo, njoo kwangu uso kwa uso na usimame. Hebu—hebu tuwe na hiyo halisi, hebu njoo hapa tuone ni nani aliye sahihi na ni nani asiye sahihi juu ya hilo. Bali hawatakabaliana nalo. Kwa kweli, wanajua vizuri zaidi. Mnaona?

¹⁴⁶ Hakika, sio mimi, bali ni Roho Mtakatifu, Malaika yule yule wa Mungu mnayemwona. Vipi kuhusu siku hizi hapa wakati mambo haya yote yametukia, na Malaika huyu wa Bwana akisimama karibu? Nisingeyajua mambo haya, bali huu ndio ule wakati, uko hapa. Tutakapozipitia Roho hizi saba, zile pembe saba, na kadhalika, leo hii, Bwana akipenda, mtaona mahali lilipo. Ni—ni majira tuliyomo ambapo funuo hizi zinapaswa kuja. Ni Kitabu cha mafunuo, ufunuo wa Yesu Kristo. Nasi tuliona, mlango wa kwanza kabisa, Yeye alifunua Yeye alikuwa

ni nani. Na sasa Yeye anaichukua ile Mihuri Saba, akifunua jinsi alivyoikomboa dunia.

¹⁴⁷ Na moja yake ilikuwa ni kwa Jina la Yesu Kristo. Hiyo nyingine ilikuwa ni kuwaondolea watu hofu, kama vile: Milele, ukombozi wa Milele, kuhesabiwa haki kwa imani, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na kitu gani? Kwamba tuko salama Milele, akiyaondolea mbali mashaka yote kutoka kwa watu. Iwapo unayo arabuni ya wokovu wako, Mungu tayari amekutia muhuri hata siku ya ukombozi wako. Waefeso 4:30 inasema:

...msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye ninyi mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu.

¹⁴⁸ Sasa, utarudije—utarudije nyuma? Huenda ukarudi nyuma, bali huwezi kupotea. Na kama ukikaa katika hali hiyo, inaonyesha kwamba hukuwa Naye tangu mwanzo. Lakini endapo wewe ni mwana wa Mungu, “Mwabuduo akiisha kusafishwa mara moja hawezi kujiona tena kuwa ana dhambi,” inasema Waebrania. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo huwezi—huwezi kuwa Mkristo, huwezi kuwa na Roho Mtakatifu na kukimbia nje na kuishi ulimwenguni. “Ukipenda ulimwengu, mambo yaliyo katika ulimwengu, kumpenda Mungu hakumo ndani yako.” Kwa hiyo unaikiliza tu sauti ya uongo mahali fulani, ibilisi amekutia majivuno. Bali kama ukiyachunguza maisha yako kwa Neno la Mungu na inaonyesha ya kwamba unaishi moja kwa moja chini kwenye kurasa za Biblia hiyo, basi unao usalama wa Milele.

¹⁴⁹ Wala hakuna kitu cha kuogopwa. Yale Mungu aliyoahidi, Mungu atayatimiza. Ninamsai mtu yeyote kulichukua hilo. Lichukue hilo tu na kutembea pamoja na Neno hilo, kisha uone litakalotukia kwako. Ndugu, litatimiza kila kitu, Mungu alisema hivyo. Kila kitu ambacho Mungu aliahidi, kitatukia.

¹⁵⁰ Mimi...Kwa kuwa tayari nimewaambia ya kwamba kazi yangu ilikuwa ikianza, hii imekuwa ni karibu miaka kumi na mitano kuizunguka na kuizunguka dunia, na hakuna hata wakati mmoja liliposhindwa. Kwa nini? Kwa sababu, kimsingi, nilisimama juu ya ahadi ya Mungu. Nilijua ilikuwa ni Kweli. Msinfanye inilazimu kujaribu kuwaambia ni baadhi ya hekima yangu kuu, lakini Yeye Yule alieyefunua siri za moyo Ndiye hasa aliyenionyesha katika Maandiko. Maana hata sikuninii... nilipoanza kuhubiri kwa mara ya kwanza, yapata miaka thelathini iliyopita, ilinibidi kumfanya msichana rafiki yangu kuketi pale na kuisoma Biblia. Nisingeweza hata kuisoma, kwa kutokuwa na elimu nyingi. Dada Wilson, unapaswa kukumbuka hilo wakati Hope alipokuwa akinisomea Biblia kule nyuma, kuketi na kuisoma, nami ningesema, “Mmesikia yale iliyosema, fanyeni vile tu Hiyo inavyosema. Hayo ndiyo yote ninayojuu

kuwaambia.” Nao wote waliofanya hivyo, mbona, wakawa sawa. Hivyo tu. Ninge—ninge. . .

¹⁵¹ Yeye angesema, “Mungu aliupenda sana ulimwengu akamtoa Mwanawe wa pekee.”

Ningesema, “Ni wangapi wanaoamini Hilo?” “Soma yanayofuata, kipenzi.”

“Akamtoa Mwanawe wa pekee, kila amwaminiye yuna Uzima wa Milele.”

Nikasema, “Ni wangapi wanaoamini Hilo? Mnasikia vile lilivyosema.” Nisingeweza kulisoma mwenyewe.

¹⁵² Kwa hiyo, mnaona, sikuwa na njia ya kusoma kutoka shule yoyote. Lakini, loo, ninaipenda ile shule niliyoenda! Loo, huko nyuma katika pango dogo mahali fulani, huku nimemwinulia Mungu mikono yangu, siku baada ya siku namna hiyo, wakati Roho Mtakatifu aliposhuka chini katika utamu Wake na akaanza kujifunua Mwenyewe, na kusema, “*Hili ni hivi, na hivi ni hivi.*” Wala hakuna wakati mmoja mtu yeyote, kiumbe cha namna yoyote, kimeweza kuweka mikono yake juu ya lolote Lake. Na pamoja na ulokole wote na kila kitu kingine ambacho kimeenea nchini, Mungu amelishikilia Hilo juu na safi, na kulizungusha tena na tena ulimwenguni. Haleluya! Tuko katika wakati wa mwisho, ndugu. Tuko hapa kwenye wakati wa mwisho. Hivyo tu. “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Hivyo ndivyo Yeye alivyosema hasa.

¹⁵³ Sasa, ni Kitabu cha Ufunuo, Mungu akijifunua Mwenyewe. Na sasa kupitia kwa siri hizi kuu, Yeye analifunua Jina la Bwana Yesu Kristo katika ubatizo, anafunua ya kwamba hakuna kitu kama Jehanamu ya Milele (haiwezekani, hakuna Maandiko katika Biblia yanayosema kuna kitu kama hicho).

¹⁵⁴ Sasa, kuna jehanamu, na kuna ziwa la moto, na ambako waovu wanaadhibiwa, bali hatimaye wanaangamizwa. Labda miaka milioni mia kumi, bali hatimaye wanaangamizwa. Maana usingeweza kuwa na Uzima wa Milele isipokuwa umeokoka. Na kama ukiteketea Milele, huna budi kuwa na Uzima wa Milele. Mbona, akili ya kawaida ingekuonyesha hilo. Unaona? Unawezaje kuwa na wa Mile- . . . ? Ni wangapi wanaojua wakati unapokuwa na Uzima wa Milele umeokoka? Vema, kama ukiteketea Milele, hivi haitakubidi kuwa na Uzima wa Milele upate kuutambua? Kwa hiyo, unaona, hata halileti maana. Mnaona?

¹⁵⁵ Sasa, “usalama.” Wale ambao Yeye alitangulia kuwajua, aliwaita; wale aliowaita, amewahesabia haki; wao aliowahesabia haki, tayari amewatukuza. Paulo alitwambia, katika mlango wa kwanza wa Waefeso, ya kwamba “Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ametangulia kutuchagua tupate kufanywa wana wenye mamlaka kupitia kwa Kristo Yesu.”

156 Yohana anatwambia hapa katika Ufunuo, ya kwamba “Adui katika siku za mwisho, yule adui wa kidini, angeingia miongoni mwa watu na kuwa na mashirika na kadhalika, na madhehebu na kadhalika,” kama walivyo nayo siku hizi, “naye angewapoteza walio Wateule kama yamkini, naye angewadanganya *wote* ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo tangu kuwekwa misingi yenyewe ya ulimwengu.”

157 Jina lako liliwekwa lini kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kristo aliuawa lini, miaka elfu moja mia tisa iliyopita? La, bwana. Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. “Mwana-kondoo alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

158 Mnaona kile linachofanya? Ni mihuri hii ikifunguliwa, inaanwa tu kufunua mpango wa ukombozi, jinsi Yeye alivyotekeleza. Yote yamekwisha sasa, karibu tu—karibu tu kwisha. Kwa hiyo tuko katika wakati wa mwisho. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu ha—haya mambo yanafunuliwa. Vema.

159 Sasa, Mkombozi wetu wa Jamaa wa karibu anakabidhiwa Kitabu cha ukombozi kutoka kwa Mwenyewe wa asili. Mwenyewe wa asili... Wakati tulipokipoteza kwenye bustani ya Edeni, kupitia kwa Adamu, kilirudi kwa Mwenyewe wa asili. Lakini kumekuwako na jangili nchini, mkazi haramu, naye huyo ni Shetani; alikuja huku, yeye ni jangili. Dunia hii si mali yake; ni ya Mungu. Bali yeye ni jangili, mkazi haramu. Jamani, jinsi ningeweza kusema jambo fulani sasa hivi, bali afadhali nisiliseme. Ni hatimiliki ya ukombozi wetu, hiki Kitabu kilichotiwa muhuri kwa mihuri saba. Ndicho hatimiliki. Ngojeni mpaka tutakapoifikia hiyo Mihuri!

160 Yeye anaivunja mihuri, anafunua, anatupatia urithi Wake kwa watu Wake. Yeye anatoa urithi ambao Yeye alirithi, anakuwa Mkombozi wa Jamaa wa karibu, na kutupa sisi bure. Yote ilikuwa ni mali Yake. Yeye Ndiye aliyekomboa. Bali badala ya kubaki nayo Mwenyewe, anawarejeshea watu. Huo ni upendo Wake kwetu. Loo!

161 Shetani, anayeimiliki sasa, yule mkazi haramu, yeye hatimaye... Yeye hataki kuisalimisha upesi mara moja, tutaona hapa muda kidogo baadaye katika Maandiko, ninawazia huku katika mlango mwingine. Na yeye hakutaka kuisalimisha mara moja, bali ilimbidi kuipigania. Lakini, hatimaye, wakati alipoletwa kwenye shindano la kuamua, yeye alitupwa kwenye ziwa la moto. Hiyo ni kweli.

162 Yesu, Jina *Yesu* katika Injili lina sifa nne za “Mwana.” Mlijua hilo? Yesu ana sifa nne kama *Mwana* katika Injili. Moja ya hizo ni “Mwana wa Daudi”; moja ya hizo ni “Mwana wa Ibrahimu”; nyingine, “Mwana wa Adamu”; nyingine, “Mwana wa Mungu.”

163 Sasa, angalieni. Wakati Mkombozi wetu wa Jamaa wa karibu alipofanyika Yesu Kristo, Yeye alikuwa ni Mwana wa Daudi, ambaye ni Mrithi wa kiti cha enzi. Utukufu! Yeye alikirithi kiti cha enzi kwa kuwa ni Mwana wa Daudi. Mungu alisema huko nyuma ya kwamba hatamwacha Daudi kamwe “kamwe hatamwacha Daudi bila uzao.” Naye Kristo ni Mwana wa Daudi. Ndipo akawa Mkombozi wa Jamaa yetu wa karibu, huku akingojea, akipatayarisha mahali ambapo Yeye anaweza kutawala pamoja nasi. Kama Mwana wa Daudi Yeye ni Mrithi wa kiti cha enzi.

164 Kama Mwana wa Ibrahimu, Yeye ni Mrithi wa idhini ya kifalme. Amina. Hiyo ni kweli? Yeye ni Mrithi wa idhini ya kifalme (Amina!), Palestina na yote yaliyo ndani yake, “Uzao wa Ibrahimu.” Yeye alikuwa Mwana wa Ibrahimu.

165 Kama Mwana wa Adamu, ni nini Mwana wa Adamu... Mwanadamu alipoteza nini? Aliipoteza dunia. Kwa hiyo kama Mwana wa Adamu Yeye ni Mrithi wa kila kitu duniani. Haya yote anayo na Yeye hana budi kuturejeshea, ndipo Yeye anarudi jinsi alivyokuwa. Yeye ni...

166 Sasa, basi, kama Mwana wa Mungu Yeye anarithi vitu vyote. Kama Mwana wa Daudi Yeye ni Mrithi wa kiti cha enzi, kama Mwana wa Ibrahimu Yeye ni Mrithi wa idhini ya kifalme, kama Mwana wa Adamu Yeye ni mrithi wa dunia, kama Mwana wa Mungu Yeye ni Mrithi wa vitu vyote Mbinguni na duniani. Loo, jamani! Huyu ndiye Mkombozi wetu, Mkombozi wetu wa Jamaa wa karibu.

167 Sasa, tazameni! Loo, hili linanifanyia vizuri sana. Hapa ndipo kweli ni—ninapopata kulishwa. Sasa, hebu mioyo yenu iachiliwe kwa Mungu kwa dakika chache tu. Sikilizeni hili.

168 Shetani ni mkazi haramu, yeye haimiliki hii kisheria, naye amekuwa na miaka elfu mbili ya ubishi kama ndiye mmiliki ama inamilikiwa na mtu mwingine. Bali Kristo alikuja kama Mkombozi wa Jamaa wa karibu na akaikomboza iturudie. Ila Shetani anaimiliki. Lakini, mwajua, baada ya kitambo kidogo (vita hivi vikuu vikiisha) yeye atatupwa katika ziwa la moto. Mnaona? Ataangamizwa, na wote wanaoabudu pamoja naye. Lakini warithi wa wokovu watakuja pamoja na Kristo. Sasa, yeye ni mkazi haramu.

169 Sasa, kumbukeni, katika Agano la Kale, kama m—mtu aliupoteza urithi wake halafu mkazi haramu akaingia kwenye shamba lake, asingeweza kulishikilia zaidi kwa ajili ya kuangamizwa kutoka kwa mwenyewe mpaka muda wa miaka hamsini. Baada ya miaka hamsini, mwaka—mwaka wa Yubile ulikuja. Nao mwaka wa Yubile, hapo mwaka wa Yubile ulipokuja, basi kila kitu kilirudi kwenye mwanzo wake wa asili tena. Watumwa wote, walirudi kwenye mwanzo wa asili. Kama mtu alikuwa akilima shambami na baragumu ilie naye akaisikia,

angetupa jembe chini na kusema, “Mimi si mtumwa tena, narudi nyumbani kwa familia yangu.” Kila kitu kilirudishwa. Kama mkazi haramu alikuwa kwenye hiyo ardhi, ilibidi aondoke kwenye hiyo ardhi. Hivyo tu. Aliondoka kwenye hiyo ardhi kwa sababu gani? Mwenyewe halali alikuwa anarudi. Ilimbidi kuondoka.

¹⁷⁰ Haleluya! Moja ya siku hizi falme za ulimwengu huu zitaanguka, nao wenyewe halali watakuja moja ya siku hizi. Amina.

¹⁷¹ Sasa, kulikuwako na wakati ambapo ilikuwa ikibishaniwa. Kutoka siku ya arobaini, kutoka mwanzo wa siku ya kwanza ya kusafishwa kwa madhabahu, ama Kristo alipoenda Kalvari, kulikuwako na siku arobaini hata kule kupaa juu. Ilikuwa na majadiliano, kama kundi la shetani lingeichukua na kusema kwamba Yeye hakufufuka katika wafu. Walianza kutoa tangazo kule na kusema, kasema, “Wanafunzi ndio waliokuja wakamwiba Yeye usiku.” Mmesoma Biblia, “Naye akasema kwamba ‘Watu Wa—Wake walikuja wakamwiba usiku.’ Nao wakawalipa askari pesa waseme hilo.” Lakini lilikuwa likijadiliwa wakati huo, kila mtu alikuwa katika mjadala.

¹⁷² “Vema, kweli, labda ni la kimadhehebu, basi, kitu hicho chote ni chake.”

¹⁷³ Lakini kwenye siku ya hamsini ilikuwa ni Siku ya Pentekoste, ndipo Mwenyewe halali akashuka miongoni mwao (Haleluya!) akaonyesha halikuwa ni dhehebu. Kwamba ilikuwa ni kujazwa kwa Roho Mtakatifu. Hizo zilikuwa ni pesa za Mungu za arabuni kwa Kanisa Lake ya kwamba halitatawaliwa na madhehebu na kadhalika, ingekuwa ni arabuni ya ubatizo wa Roho Mtakatifu pamoja na nguvu na upendo wa Mungu. Amina! Loo, hilo si linakufanyia tu jambo fulani? Mmiliki halali! Kilikuwa wapi? Mikononi mwa Mungu. Na kwenye . . .

¹⁷⁴ Mnaona, asingeweza kuishikilia kwa zaidi ya siku hamsini. Mtasoma hilo katika—katika Mambo ya Walawi—katika Mambo ya Walawi, kwenye—kwenye sheria hizo kule. Ilisema ya kwamba wasingeweza . . . mwenyewe wa asili. Ilibidi irudi mikononi mwa mwenyewe wa asili baada ya miaka hamsini. Sote tunajua hilo. Mmesoma hilo mara nyingi, lakini . . . mnaona, “Ilibidi imrudie mwenyewe wa asili baada ya miaka hamsini.”

¹⁷⁵ Vema, basi, baada ya siku hizi hamsini-miaka, mwaka mmoja . . . siku moja ikimaanisha kama mwaka mmoja. Basi tangu ile siku ya kule kusulubiwa ambapo walichukua ninii . . . huyu Mkombozi wa Jamaa wa karibu na kumwua kwenye—kwenye siku ya Pasaka, ilikuwa ikibishaniwa wakati huo. Kanisa liliamini kufikia wakati huo ya kwamba Yeye alikuwa ni Mkombozi wa Jamaa wa karibu, “Yeye alikuwa ni Mkombozi.” Ndipo hilo lilifanya nini? Wakamwua, adui akamuua, na kusema waliuchukua mwili Wake na kuuficha mahali fulani. Na hayo

yote yalitiliwa shaka na watu, “Tlikuware Kwake? Ni jambo gani lililotukia?”

¹⁷⁶ Sasa, mwishoni mwa siku ya hamsini, basi, mnaona, lisingeweza kuwa katika ubishi tena. Ndipo, Mungu... Badala ya wao kwenda—kuendelea na kanisa lao la kiothodoksi la kale, gumu, baridi; Mungu alimtuma Roho Mtakatifu arudi, akawafukuza na kutoa wakazi haramu wote, kisha akalitwaa. Nguvu za Roho Mtakatifu zilishuka nalo Kanisa likapokea arabuni ya wokovu wake.

¹⁷⁷ Sasa, ndugu, sio kuumiza hisia zenu wala chochote juu yake, kama dhehebu ni sahihi nawe ni Mkatoliki tu kwa dhehebu, wewe ni Mbaptisti kwa dhehebu, umepotea. Mnaona, arabuni ya wokovu wetu haikuwa ni kujiunga na kanisa, arabuni ya wokovu wetu haikuwa ni kuwa mfuasi wa dhehebu fulani. Arabuni ya wokovu wetu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu pasipo na dhehebu lolote! Amina.

¹⁷⁸ Wasingeweza kuishikilia kwa ajili ya jambo hilo, kupita siku hiyo ya hamsini, maana hiyo ilikuwa ni siku ya Yubile wakati kila kitu kilirejeshwa kwa mwanzo wake asilia. Nazo ngu—nguvu za Mungu zilirudishwa kwenye asili yake, siku ya hamsini, ule mwaka wa Yubile wakati vitu vyote viliporejeshwa.

¹⁷⁹ Sasa, utakuja mwaka mwingine wa Yubile na, huo, tumekuwa nao yapata tu wakati huu. Kama uliona, Pentekoste imekuwa ikishuka Marekani kwa yapata miaka hamsini, mahali fulani kwenye muda huo. Yapata tu miaka hamsini iliyopita Pentekoste ilianza kushuka. Sasa kinachotukia, kanisa linapokea Kitabu kilichotiwa muhuri kwa mihuri saba cha ufunuo wa Yesu Kristo (cha Mihuri Saba) wala si hata moja juu ya kumi yao wanaweza kukipokea.

¹⁸⁰ Lakini unapoanza kuuona mwaka wa Yubile ambako haitubidi kubishana na kuzozana na kuvutana namna hii, bali tayari tuko salama katika Kristo! Tayari tunalo Jina la Bwana Yesu Kristo katika ubatizo. Tunazo siri hizi zote kuu tutakazozileta kwenye Mihuri hii Saba, na kuwathibitishia ya kwamba hiyo ilikuwa ni mihuri iliyotiwa muhuri kutoka kwenye macho ya watu. Mungu akiwa ni msaidizi wangu, nitawathibitishia ya kwamba hawangeweza kuona Hilo kwa Biblia (Halafu, hakika, kama Biblia ilisema hivyo wewe utaiamini.), kwamba hawangeweza kuona chochote ila “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” mpaka wakati huu. Hawangeweza kuona ya kwamba hakukuwako na jehanamu ya Milele, mpaka wakati huu. Hawangeweza kuona kulikuwako na usalama wa Milele chi-... Ninamaamisha kwa mwaminio halisi. Hakika, kumekuwako na dhihaka yake kotekote, sauti isiyojulikana wanayotoa. Hiyo ndiyo sababu watu... Wao wanasema, “Mbona, waangalieni hao Wapresbiteri na kadhalika, wanavuta sigara, wanakunywa pombe, na kila kitu kingine, na kusema

wana usalama wa Milele.” Naam, lakini, mnaona, hiyo ni—hiyo ni kuitupilia mbali ile Baragumu halisi.

¹⁸¹ Hebu tutafute kujua Hapa nyuma na tuone kama Baragumu hulia, kama hurudi moja kwa moja kwenye Mwanzo hadi Ufunuo, mbele na nyuma, wakati muhuri huu utakapofunuliwa; mnaona, mambo haya yakifunuliwa.

¹⁸² Sasa, loo, ndugu! Nilidhani nilikuwa tu...Itanibidi kuliachilia mpaka wakati mwingine nitakapokuja huku. Nina karibu kurasa sita hapa bado; ama—ama, sawa, la, tuna ibada ya ubatizo inayokuja. Hebu nisome hili, baadhi ya mambo haya madogo papa hapa, ule mwaka wa Yubile. Vema.

¹⁸³ Sasa, nyinyi—nyinyi nyote mnayaandika Maandiko? Katika Yeremia 32, na tuanzia kwenye kifungu cha 6 kama mkinini. . . nanyi mtakapofika nyumbani, ninataka mwisome. Sasa, Yeremia, kuwafanya muone gombo hili ni nini, nitalitoa hili. Hebu tulichukue hili gombo, kwa vyovyote vile. Hiyo itanipa kama dakika zingine kumi, za lile gombo. Sasa, mnakumbuka, Kitabu hiki kilitiwa muhuri. Sasa, kitabu katika nyakati za Biblia hakikuwa ni kitabu cha pembe nne kama *hiki*. Kilikuwa ni kitabu namna *hii*, ambacho kiliitwa kitabu, “gombo.” Ni wangapi wanaojua hilo? Um-hu. Hakika, kilikuwa ni gombo. Vema.

¹⁸⁴ Sasa, Kitabu hiki—hiki kilitiwa muhuri kwa mihuri saba. Sasa, Hicho kilikuwa ni Biblia Nayo ilitiwa muhuri kwa mihuri saba. Basi sasa angalieni jinsi hili lilivyotendeka.

¹⁸⁵ Yeremia, wakati yeye—wakati alipokuwa akienda kuwa. . . yeye alikuwa ametabiri ya kwamba angechukuliwa mateka. Katika Yeremia sasa, mlango wa 32. Yeye alikuwa anaenda kuchukuliwa mateka huko Babeli, walikuwa wanaenda kuwa kule kwa muda wa miaka sabini. Alikuwa ametabiri hilo. Nanyi wasomaji wa Biblia mmeipitia mara nyingi. Naye alikuwa anaenda kuchukuliwa kule kwa muda wa miaka sabini. Na yeye—yeye kwa kweli alikuwa ndiye jamaa wa karibu sana kwa hayati binamu yake. Binamu yake (H-a-n-a-m, e maradufu, l) Hanameel, Hanameel, Hanameel, alikuwa ni. . . jamaa yake wa karibu. Kwa hiyo yeye alijua ya kwamba—ya kwamba adui angeshikilia—angeyashikilia ma—makaratasi na kadhalika ya mahali pake, lakini wakati. . . Alijua ya kwamba Mungu kamwe asingeweza kuwaacha watu Wake, kwa hiyo wakati watakaporudi, apate kuwa nayo na awe mwenyewe halisi wa ule urithi, hivi ndivyo alivyofanya: aliyaandika yote.

¹⁸⁶ Ni wangapi wamewahi kulisoma? Vema, mmelisoma, mmelisoma basi. Vema. Sasa, yeye aliyachukua na kuyatia muhuri jinsi hasa magombo haya yalivyotiwa muhuri hapa. Ni jambo la kuvutia mno, la ajabu sana ulilopata kuona.

¹⁸⁷ Sasa, nitajaribu kulionyesha kwa mfano kwa kipande hiki cha karatasi, sijui kama ninaweza ama siwezi. Sasa, hivi ndivyo

kilivyoandikwa, namna *hii*. Sasa, yeye alifanya hivyo na kukitia muhuri namna *hii*, kila kimoja. Sasa, kilichotukia, juu ya kila mmoja wa mihuri hii kuliandikwa hapa urithi wake na yale yaliyotukia, na wale wote walioaga kabla yake na jinsi alivyokuja kuurithi. Yote yalitiwa muhuri namna *hiyo*.

¹⁸⁸ Sasa, hivyo ndivyo Mungu amekiweka Kitabu Chake kilichotiwa muhuri kwa mihuri saba. Sasa, vile tu Yeye anavyourarua huu, huo ufunuo unarudi moja kwa moja na unaenda kote kote hadi upande wa nyuma wa kile Kitabu. Hiyo ndiyo sababu unaweza kulichukua Jina la Yesu Kristo na kulifuatilia kutoka Mwanzo hadi Ufunuo na kuonyesha hakuna kitu kama “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Mnaona? Mnaona, unaenda kote kote kwenye Biblia, Hiyo inalifunua.

¹⁸⁹ Kisha unachukua kama, “Kuna jehanamu ya Milele.” Unalivuta hilo na kulifuatilia kote kote; kamwe hapajakuwapo na jehanamu ya Milele, maana hapo mwanzo Mungu alisema kwamba jehanamu *iliumbwa* kwa ajili ya ibilisi na malaika zake, kwa ajili ya adhabu yao ya usoni. Basi kama jehanamu ni ya Milele, ingewezaje kuumbwa? Neno uumbaji kamwe halikuninii... Neno *Milele*, “hakikuanza kamwe wala kamwe hakiwezi kwisha.” Basi daima kulikuwako na jehanamu endapo ni jehanamu ya *Milele*, “jehanamu ilikuwako wakati ule ule wote, wakati ule ule kulipokuwapo na Mungu kulikuwako na jehanamu, kabla hapajakuwapo na dhambi yoyote kungali kulikuwako na jehanamu.” Huh! Loo, jamani! Mnaona, huwezi kufaulu.

¹⁹⁰ Kwa hiyo angalieni wakati mambo haya yakijifunua yenyewe, linarudi moja kwa moja na kukifungua hiki Kitabu. Kwa hiyo kwa kweli hili linatoa picha nzima ya Biblia, nayo ile mihuri ambayo imeificha Biblia hii kutoka kwenye macho ya wenye hekima na akili. Mungu, kwa Roho Mtakatifu, anaifungua namna hii na kuifunua moja kwa moja kote katika Biblia. Utukufu kwa Mungu!

¹⁹¹ Ndugu, nawaambia, hilo linafanya mtindo wa—wangu wa ulaji wa kiroho kulisimkwa. Mnaona? Mnaona? Sasa, angalieni hapa! Mnaona, ni—ni mu-...kama...Mnaelewa ninalomaanisha? Mnaona, huu hapa, muhuri. Sasa, kama ukiangalia na kusoma hapa, nenda kwenye Yeremia na kuona jinsi a—a—a—alivyolitia muhuri.

¹⁹² Sasa, hicho hapo Kitabu, kimeandikwa mle ndani. Sasa, kwenye wakati tu wa ufunuo wa kwanza, ndipo Yeye anaufungua muhuri huu. Sasa, tazameni muone kile muhuri huo wa kwanza ulichokuwa tutakapoifikia Mihuri. Kisha wakati wa muhuri wa pili, Yeye anaovuta muhuri huo mwingine unatoka. Nanyi mnajua mahali tulipo? Tuko karibu sana na ule muhuri wa saba sasa hivi. Ndipo wakati ule wa saba...

¹⁹³ Wakati muhuri wa kwanza ulipofunguliwa, baragumu ya kwanza ilitoa sauti yake na pigo la kwanza likaanguka. Wakati muhuri wa sita ulipofunguliwa, wa sita ulitoa sauti yake nalo pigo la sita likaanguka. Liangalieni tu, ndilo jambo zuri kuliko yote mliyowahi kuona. Basi nitakapofanya hivyo, nitajitafutia ubao mkubwa mno wa kuandikia, niulete hapa na kufundisha moja kwa moja hapa, kwa hiyo tutachukua tu wakati mwingi kwenye kila muhuri kisha turejee nyuma na kuichukua historia na kadhalika, na kuthibitisha wakati hasa lilipotukia, na kuonyesha moja kwa moja hapa katika Biblia wakati iliposema lingetukia, na papo hapo wakati lilipotukia, tarehe tu na kila kitu kingine. Nililipata, amina, nililipata kutoka Kwake. Hiyo ni kweli. Hiyo hapo hiyo mihuri.

¹⁹⁴ Sasa, wakati Yeremia alipokiandika kitabu hiki, kilitiwa muhuri... Hili hapa jambo zuri ninalowataka mlione, ninyi nyote mnaolisoma, kwamba hivyo vitabu vilivyotiwa muhuri... Sasa, kumbukeni, yeye ataondoka. Alikuwa ametabiri. Sasa, hakujua hilo, ila tu kwa unabii. Mnanifuata? Kwa unabii yeye alijua, kupitia ufunuo wa Mungu, ya kwamba wataondoka kwenye nchi hiyo kwa muda wa miaka sabini. Mnamkumbuka yeye akitabiri hilo? Yeye angekuwa na miaka sabini, wangekuwa katika utumwa. Kwa hiyo alitaka kuwa na hakika ya kwamba muhuri huu (kwamba urithi wake) ungewekwa, maana alikuwa na... aliurithi urithi wa binamu yake. Kwa hiyo akaandika wote, kisheria. Naye alifanya nini nao? Kusudi usioze wala kuingia kutu, aliuweka katika chombo cha udongo; na kuuhifadhi usije ukaoza wala kuingia kutu, hata miaka sabini ilipokwisha.

¹⁹⁵ Utukufu kwa Mungu! Nilitumaini mngelipata! Mnaona kile Mungu alichofanya? Yeye hakulifunua kwa wenye hekima na wenye elimu (kusudi wakalibishanie Hilo kwa wakati huu wote), bali aliuweka katika Chombo cha udongo Naye akajiumbia Mwenyewe Mwana Wake, Kristo Yesu. Na katika siku hii ya mwisho sasa Yeye anaifungua ile mihuri na kuionyesha kwa Kanisa Lake. Ukawekwa kwenye Chombo cha udongo usije ukaoza wala kuingia kutu! Haleluya! Loo! Ninajua mnafikiri mimi ni mtakatifu anayejibingirisha. Labda ndivyo nilivyo. Mnaona? Lakini Hilo hapo! Umewekwa katika Chombo cha udongo kilichokombolewa kutoka duniani, kikafufuka kwenye asubuhi ya Pasaka ambapo mihuri ya mauti isingeweza kumshikilia Yeye tena; lakini aliivunja mihuri na kufufuka, huku akijithibitisha Mwenyewe katika siku hizi za mwisho ya kwamba Yeye yu hai! Yeye yuko Kanisani Mwake! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nalo hilo limefichwa kutoka kwa seminari, limekuwa limefichwa kutoka kwa madhehebu.

¹⁹⁶ Na katika siku hizi za mwisho Yeye analifunua kwa Uwepo Wake Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Yeye humchukua mtu ambaye anaweza kuutoa ulimwengu ndani yao na vitu kutoka kwao (ukanisa kutoka kwao), kusudi Yeye

aweze kuzungumza kupitia kwao na kufunua na kuifungua mihuri hii namna hii Mwenyewe. Mnaona? Haleluya! Loo, hivi hamupendi? Jamani, jamani, jamani!

¹⁹⁷ Mpango wetu wa wokovu, ule ule sasa ukifunuliwa ndani ya Yesu Kristo. Yeye aliufunuaaje katika siku hizi za mwisho? Kupitia kwenye kufunua Kwake muhuri. Mbona, hakuna mtu... Kamwe hukulisikia limeandikiwa juu yake maishani mwako kuhusu Uzao wa Ibrahimu, jinsi walivyopitia katika kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; jinsi ambavyo malaika huyo angeingia katika siku za mwisho, aelekeze mgonjo wake kwenye kusanyiko na kusema yale hasa Sara aliyokuwa akiwazia moyoni mwake mle ndani (hilo halikutukia hadi siku hii, hiyo ni kweli, hii ndiyo siku); na imani ya Ibrahimu; na Jina la Bwana Yesu.

¹⁹⁸ Sasa, jambo moja hapa, ninayo hapa mambo matano ningetaka kuyazungumzia, kwa sekunde moja tu, upesi tu niwezavyo. Angalieni. Ile saba... Kunayo mihuri saba, na kuna saba tano katika mpango wa Mungu wa ukombozi. *Tano* ni namba ya “neema.” Ni wangapi wanajua hilo? J-e-s-u-s, i-m-a-n-i, tano ni namba ya neema. *Sita* ni siku ya mwanadamu, na *saba* ni siku ya—yake ya ukombozi.

¹⁹⁹ Sasa, tazama. Sasa, kunayo mihuri saba katika huu, ama—ama hatua saba katika mpango huu mkuu wa ukombozi. Kuna nini saba? Mihuri saba ya ukombozi, Roho saba za Mungu... Tunaona ya kwamba (kama ukitaka kuona kama linasema, “Roho Saba,” hebu nione hapa kwa dakika moja), mlango wa 5, kuanzia kifungu cha 6 (ninaamini, tunaona hapa), kifungu cha 6:

Kisha... tazama, tena, nikaona, katikati ya kile kiti cha enzi na wale wenye uhai wanne, na katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye vichwa saba na macho saba, ambazo ni Roho saba za Mungu zilizotumwa katika dunia yote.

²⁰⁰ Hizo Roho saba ni nini? Hao wajumbe saba. Kuna Mtakatifu Columba, na Ireneo, na—na John Wesley, na Martin Luther, na kadhalika. Mnaona, “zile Roho saba,” ambazo ni watu saba (malaika saba), ambazo ni jumbe saba.

²⁰¹ Mihuri saba, Roho saba, malaika saba, pembe saba, na makanisa saba. Mnaona, saba saba, kuna saba tano, ambazo, *saba* ni “ukamilifu,” *tano* ni “neema,” Neema ya Mungu kwa Nyakati Zake Saba za Kanisa. Watu Wake saba wajumbe, Roho Zake saba za Mungu, ile mihuri saba iliyopangiwa ya ukombozi (tuko ndani yake sasa hivi), zile *pembe* saba zinamaanisha “nyakati” saba.

²⁰² Maana, *pembe* inamaanisha “ufalme.” Mnakumbuka ile taji iliyokuja juu ya yule mnyama (pembe) katika Danieli, na kadhalika? Mnaona, inamaanisha ufalme, ama “nyakati saba.”

Basi, kumbukeni, Yesu alisema, “Wengine walilala usingizi kwenye zamu ya kwanza, wakati mmoja; mwingine kwenye zamu iliyofuata, wakati uliofuata; mwingine; na mwingine; moja kwa moja hadi kwenye zamu ya saba. Ndipo katika zamu ya saba Bwana-arusi akaja, ndipo hao wote wakaamka.” Mnakumbuka hilo?

²⁰³ Kwa hiyo ni “nyakati” saba zilizokuwa zile *pembe* saba, nayo *makanisa* saba, ama “ninii saba . . . vipindi vya nyakati za mwili wa waaminio.” Loo, ni kamilifu tu iwezavyo kuwa. Yereimia . . . Jamani, “kile Kitabu,” “nyakati,” jinsi ilivyokombolewa! Jinsi . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . papa hapa.

²⁰⁴ Ule wa saba na wa mwisho wa mihuri hii, itakapofunuliwa, inapatikana katika Ufunuo mlango wa 10, kulikuwako na Malaika mwenye nguvu (ambaye alikuwa ni Kristo) aliyeshuka na kuweka mguu mmoja juu ya nchi na mmoja juu ya bahari, na kuinua mkono Wake na kusema, “Siku imekwisha. Wakati umekwisha. Yote yamekwisha. Hapatakuwa na wakati baada ya haya.”

²⁰⁵ Naye akasema, “Wakati wa kupiga ninii . . . kwenye wakati huu, siri ya Mungu itatimizwa.” Kwamba Mungu ni nani na jinsi alivyodhihirishwa; jinsi wakati muhuri huo ulipofunguliwa, jinsi ambavyo tunaanza kufahamu sasa jinsi Yeye alivyokuwa ni Mwana wa Mungu, Yeye alikuwa ni Mungu Mwenyewe aliyefanyika mwili; na ufunuo wa kwamba Yeye ni Nani; huo unapaswa kutimizwa kabla Malaika huyu hajaweza kuuweka mguu Wake juu ya nchi na bahari na kuapa kwamba “hakutakuwako na wakati baada ya haya” hapo wakati huu utakapowadia. Tuko kwenye huo uga wake wa mbele sasa hivi. Mnaona?

²⁰⁶ La mwisho ya hayo ni Ufunuo 10, “Mguu juu ya nchi na juu ya bahari,” wakati ulikuwa umekwisha, ukombozi umekwisha, na sasa Yeye anaingia kama Simba. Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo wakati ule, sasa anaingia kama Simba wa kabila la Yuda.

²⁰⁷ Sasa, hebu nisome tu haya yaliyosalia kusudi niweze kuwapa ninyi upesi sana sasa, na kifungu cha 8:

Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale ishirini na . . . na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, . . . na maombi ya wale watakatifu.

²⁰⁸ Sasa, huu ni wakati ambapo kila kitu hakina budi kuabudu. Sasa, kumbukeni, jinsi linavyofaa. Sasa, msiache tulikose hili sasa. Sikilizeni kwa makini. Wakati siri zote za wakati wa kanisa zilipokwisha, wakati siri zote za mpango wa ukombozi, hiyo mihuri saba ilifunguliwa kwenye. . . mara baada ya jambo hili sasa, tazameni, ni wakati wa—wa vyote, kila kitu Mbinguni

na kila kitu duniani kumwabudu Mungu. Sasa, angalieni kile kinachotukia. Sikilizeni hili...ni, sikilizeni tu hili kwa dakika moja:

Nao wakaimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe...

209 Sikilizeni hii ilikuwa ni ibada ya jinsi gani! Wale wazee, wenye uhai, kila kitu kilianguka moja kwa moja mbele Zake, mnaona, jinsi hiyo, wakati alipofanya mpango Wake mkamilifu. Ni wakati wa kuabudu sasa, mnaona:

Nao wakaimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake: kwa maana ulichinjwa, na umemnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila,...lugha, na jamaa, na taifa;

Na Wewe umetufanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu: nasi tutamiliki juu ya nchi. (Sikilizeni, hao watu waliokombolewa wakilia huko nje. Hmm!)

Nami nikatazama, nikasikia sauti ya malaika wengi pande zote za kile kiti cha enzi, na za wale wenye uhai na za wale wazee: na idadi yao ilikuwa ni elfu kumi mara elfu kumi, na maelfu ya maelfu; (Kila kitu Mbinguni kinamwabudu Mwana-Kondoo huyu, mnaona.)

Wakisema kwa sauti kuu, Astahili Mwana-Kondoo (Haleluya! Haleluya!) aliyechinjwa, kuupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka.

210 Sikilizeni, “Na kila kiumbe!” Sikilizeni yale Yohana aliyofanya:

Na kila kiumbe kilicho mbinguni na juu ya...nchi, na chini ya nchi, na juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, vilinisikia (Yohana) nikisema, Baraka,... heshima,... utukufu,... uweza una yeye aliyeketi juu ya kiti cha enzi, na kwa Mwana-Kondoo, hata milele na milele.

211 Hapana shaka Yohana kweli alikuwa na Pentekoste yake mwenyewe. Yeye alisema, “Kila kiumbe Mbinguni, na kila kiumbe nchini, kila kiumbe chini ya nchi, kila kiumbe kilichokuwa baharini, kilinisikia nikisema, ‘Amina, utukufu, heshima, uweza, na baraka, ziwe na Yeye aketiye juu ya Kiti cha Enzi, yule Mwana-Kondoo.’”

212 Wakati wa kuabudu! Amina! “Walifanyaje jambo hilo?” Hili hapa Neno Lake, wewe...wote walilisisikia.

Na wale wenye uhai wanne wakasema, Amina. Unasema kweli, Yohana, piga makelele tu na umsifu Yeye kwa sauti kuu uwezavyo. Ni...

...vilinisikia *nikisema*, Baraka, Amina, *utukufu*, hekima, *nguvu*, na uweza...

...Na wale wazee *ishirini na wanne wakaanguka*, *wakamsujudu yeye* aliyeketi...*aliye hai milele na milele*.

213 Ni hadithi nzuri jinsi gani! Sasa, sina wakati. Nimeandika, muktadha fulani juu yake hapa, bali mkutano wetu ujao kabla hatujaliingilia hili... Labda nitakapotoka kwenye likizo yangu ama wakati mwingine, ninataka kuyachukua haya majuma sabini ya Danieli na kuyafunganisha mumu humu, na kuonyesha mahali yanapolipeleka kwenye Yubile ya Pentekoste, na kuyarejesha moja kwa moja pamoja na vile ninii saba... hiyo mihuri saba itakayofunguliwa hapa kabla tu hatujaenda, na kuonyesha kwamba ni wakati wa mwisho, hii...

214 Mwana-kondoo, yule Masihi, Mtawala atakayekuja naye anapaswa kuwa kwa ajili ya majuma sabini (hiyo ni miaka saba) iliyotabiriwa kwa watu Wake. Naye yule Mtawala angekatiliwa mbali katikati, hiyo ni mitatu na nusu, ile nusu ya saba ni tatu na nusu, angekatiliwa mbali. Nayo sadaka ya kila siku ingeondolewa; na lile chukizo la uharibifu (ambalo Uislamu wa Omar ulisimama kwenye eneo la hekalu wakati walipolitekteza hekalu), halafu kuna ile miaka mitatu na nusu bado iliyosalia kwa Israeli.

215 Naye Kristo alikuja akahubiri miaka mitatu na nusu hasa, nayo sadaka ya kila siku ikaondolewa, kila kitu kikamilifu tu kilivyoweza kuwa. Nao Uislamu wa Omar ulikuwa papo... ulijengwa juu ya uwanja ule ule na unasimama hadi wa leo. Nao watazikanyaga kuta za Yerusalemu hata kipindi cha wakati wa Mataifa kitakapomalizika, Kanisa litwaliwe juu (walio Wateule, Bibi-arusi) kutoka huko.

216 Ndipo wale manabii wawili, Eliya na Musa, wanawaendea Israeli kwa hiyo miaka mingine miwili na—miwili na nusu... miaka mitatu na nusu. Ndilo jambo la kupendeza kuliko yote wakati ukiliona likielezewa.

217 Mnampenda? Kwa mioyo yenu yote? Mnaelewa sasa kile Kitabu kilichotiwa muhuri kwa mihuri saba kilichokuwa? Jambo ni kwamba: tunacho, "katika gombo," sasa. Basi kumbukeni tu, katika siku hizi za mwisho tu... Kiliwekwa kwenye Chombo cha udongo. Mnaelewa hilo sasa? Nacho hicho Chombo cha udongo kilikuwa ni Nani? Yesu Kristo. Hakuna mwanadamu aliyekuwa Nacho, hakuna mtu aliyekuwa Nacho, ni kupitia Yeye tu. Hata halikuandikwa katika Neno. Kama lilikuwa limeandikwa katika Neno, lilifichwa sana hata usingeweza kulipata. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo linafunuliwa ndani Yake, na kwenye Chombo hicho cha udongo kusudi lisioze.

218 Ndipo Yeye anakuja na kulivuta nyuma moja kwa Kanisa Lake, na kusema, "Mnaona, ni mimi yeye yule jana, leo,

na hata milele. Mnaona? Mnaona? Sasa, daima mmeshangaa kama—kama maskini mwenye dhambi atateketezwa Milele ama ataangamizwa tu baada ya miaka milioni moja. Hili hapa. Hivyo ndivyo ilivyokuwa. Hakuna kitu kama jehanamu ya Milele. Isingeweza kuwa ni ya Milele, maana mimi... jehanamu haikuwapo pamoja na Mimi wakati nilipoanza huko nyuma. Niliiumba nipate kuwaadhibia waovu mle. Mnaona? Mnahofu nini sana hivi, mnaona, kuhusu Uzao wa Ibrahimu na mambo hayo yote mbalimbali? Ninii tu...” Huo ni ninii tu—ni muhtasari wake tu, mnaona, lakini unapoingilia jinsi Mungu anavyoifungua hiyo mihuri, na kuionyesha, ushuke moja kwa moja; unaona, unapofanya hivyo, basi huwezi kukiondokea Kitabu hiki. Hiyo mihuri...

219 Unasema, “Loo, muhuri ulimaanisha jambo lingine, Ndugu Branham.”

220 Ngoja kidogo! Haina budi kulingana na Hiki, kwa maana kilitiwa muhuri upande wa nyuma wa hiki kipate kukifunua Hiki. Ni... Ni kitu gani? Ilikuwa ni nini? Hapa, kama hapa, Yeremia. Unasema jambo *fulani-fulani* lilitukia; unavuta *hili* nje, hapa ndipo hilo lilipo. Vema. Urarue *huo* na kuangalia huku nyuma, hapa ndipo iliposoma kilichotukia. Vema. Unararua *huu* kutoka hapa, uangalie hapa, na hilo ndilo lililotukia. Unaona, hilo ni jambo lile lile kilicho Kitabu hiki, mnaona, upande wake wa nyuma.

221 Wao wanasema, “Vema, siwezi kuelewa. Wengine walisema, ‘Baba, Mwana,’ na wengine, ‘Roho Mtakatifu,’ na wengine wakasema, ‘Jina la Yesu,’ kila kitu namna hiyo.”

222 Imefichwa miaka hii yote. Lakini sasa hili hapa, linarudi moja kwa moja nyuma, linarudi moja kwa moja kuonyesha kunaye Mungu mmoja pekee. Kamwe hapakuwapo ila na Mungu mmoja. Hiyo ni kweli. Nalo Jina Lake...

223 Ni kama Kitabu cha Mathayo, 28:19, “Enendeni basi, mkayafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” na Baba si jina, na Mwana si jina, na Roho Mtakatifu si jina. Sasa, mtawabatizaje? Ni lipi kati ya hayo majina mtakalobatizia, wakati hakuna moja la hayo lililo majina? Nini basi? Hutabatiza katika jina lolote, basi. Hiyo ni Shule ya Manabii tena, mnaona.

224 Kisha unarudi mahali hapa huku, nawe unapachukua hapa na kuparejesha nyuma na kurudi kwenye Mathayo 1, Yeye angefanya nini? Alilirejesha tu hilo moja kwa moja nyuma na kulirudisha hapa nyuma:

Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi: (Sio Mungu watatu, sasa, mnaona.) Wakati... mama yake... alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mtoto wa Roho Mtakatifu. (Sio Mungu Baba; “Roho Mtakatifu.” Huh?)

...yote hayo yamekuwa, ili...

Basi Yusufu mumewe...vile alivyokuwa mtu wa haki,...asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri.

...mambo hayo...alipokuwa akifikiri...tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu...kumchukua Mariamu mkeo: maana mimba yake ni kwa uweza wa...(Mungu Baba?)...Roho Mtakatifu.

225 Nilifikiri, "Mungu Baba alikuwa ndiye baba Yake." Ninasema hili kwa sababu ya ubatizo unaokuja. Mnaona? Nilifikiri, "Mungu Baba alikuwa ndiye baba Yake." Sasa, ama Roho Mtakatifu na Mungu Baba ni Mmoja, la sivyo Yeye alikuwa na baba wawili; basi Yeye ni mtoto haramu, na basi tuna Mungu wa aina gani? Hmm? Mnaona?

Basi hayo yamekuwa...yote...yamefanywa, ili litimie...lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii...

...bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana,... watamwita jina lake Yesu,...(Hiyo ni kweli?)...Naye ataitwa Imanueli, maana...yake, Mungu pamoja nasi.

226 Sasa, mnaona, wakati alipouvuta nyuma ule muhuri, kitu hicho chote ni nini kutoka Mathayo mlango wa kwanza (kurudi nyuma)? Mbona, Yesu Kristo. Hivyo ndivyo Petro alivyosema hasa kwenye ile Siku ya Pentekoste. Hivyo ndivyo hao wengine wote walivyosema.

227 Hakika, ilibidi kundi hili la Warumi kuja na kusema, "Loo, la! hatuna budi kuwa na Mungu watatu. Hatuna budi..." Wanao elfu kumi wao sasa: kuna akina Mariamu na akina Mtakatifu Cecilia, na Mtakatifu Marcus, na Mtakatifu *Fulani-wa-fulani*. Nami nafikiri kuna mia tano na kitu huko kwenye Jiji la Meksiko. Mwanamke mmoja aliuawa wakati fulani uliopita na baadhi ya wapenzi wake, nao wakaanza kumpigania hata wakamuua, kwa hiyo wakamfanya mtakatifu, na watu wanafanya vitubio kwake, na kila kitu namna hiyo. Kuamini mizimu!

228 Na hapa kanisa la Kiprotestanti linakuja huku na ile wanayoiita Kanuni ya imani ya Mitume, "Ninaamini katika Mungu Baba Mwenyezi, mhifadhi wa mbingu na nchi, na ninii—na kanisa Katoliki Takatifu la Kirumi. Pia ninaamini katika uombezi wa watakatifu, ushirika wa watakatifu." Waprotestanti wakikariri chini ya kiapo cha Mungu, ya kwamba anaamini katika ushirika wa watakatifu. Huko ni kuamini mizimu! Mnaona? Kisha wanaendelea na kufanya jambo hilo, hakika, kwa sababu kanisa lilisema hivyo. (Ee Mungu, jinsi nilivyo na furaha kujua yale nijuayo! Jinsi nilivyo na furaha kujua yale nijuayo!) Bila kutambua wanajitia muhuri moja kwa moja

wakijiondoa kwa Mungu, wakaingia huko nje gizani. Wala huwezi kuwaambia, kwa sababu kabisa hawawezi kuliona.

229 Ninataka kuuliza...hakuna mtu anayepaswa kusema hili. Kunao angalau watu kumi na watano ama ishirini, wanaoketi papa hapa, waliokuwa na hatia ya kuwazia ya kwamba mimi nilikuwa ni Yesu Kristo. Wangewezaje kufanya jambo hilo? Nilikuwa nikiwakemea sana mpaka nikaona kwamba Mungu aliniambia “ilikuwa ni roho fulani.” Nao hao watu, nikasema... Nao hao watu waliniamini, kila neno. Nikasema, “Mtaniamini vipi basi, nikiwaambia?” Basi tukaingia kwenye Neno, ndipo wakaanza kuona, kasema, “Vema, hakika, hatukukuamini la sivyo tungalisikiliza yale uliyosema.” Mnaona hapo?

230 Lakini kweli walidhani walikuwa sahihi, waaminifu. Mnaona? Basi mmoja wa hao roho akikupata, aliye nalo, unaona, utaliamini kabisa. Sijali, wewe...hakuna mtu anayeweza kukwambia vinginevyo. Unaona? Haidhuru ni kiasi gani Neno linasema hivyo, vema, wewe huliamini tu kwa vyovyote vile; unaendelea tu. “Ukitaka kuwa hivyo, endelea, nami nina njia yangu mwenyewe.” Mnaona, hiyo inaonyesha umetiwa mafuta na roho mbaya.

231 Roho wa Mungu dai-...Vema, unasema, “Vipi kuhusu wewe mwenyewe, Ndugu Branham?”

232 Ninamwomba mtu yeyote...Sikuzote niko tayari kwa mtu yeyote kunionyesha yaliyo kweli na ya uongo, bali halina budi kuwa ni Neno. Hawawezi kusema...Halina budi kutoka kwenye Neno! Basi hapo ndipo mihuri hii inapofunguliwa. Na kamwe msihofu, iwapo ni muhuri utajitangaza wenyewe kutoka Mwanzo hadi Ufunuo. Kwa hiyo hiyo hapo ile mihuri. Hivi hamumpendi?

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

233 Na tuinamishe kichwa chetu. Ni wangapi humu ndani wasiomjua kama Mwokozi wenu, ungetaka kumdai Yeye moyoni mwako? Mnajua, ninaamini katika kwenda madhabahuni, kweli ninaamini hilo. Hilo ni jambo zuri. Bali katika Biblia kamwe hawakuenda madhabahuni wakaokoke, waliliamini tu moyoni mwao na kulikubali. Ni wangapi wenu watakaokuja kwa njia ya Biblia, “Wote walioamini walibatizwa”? Ni wangapi wanaoamini leo, kamwe hawajafanya hilo hapo kabla bali wanataka kukiri hadharani ya kwamba ulikuwa “makosani” katika njia zako, nawe unataka kumkubali Yesu kama Mwokozi wako? Mwaweza tu kuinua mikono yenu huku vichwa vyenu vimeinamishwa, msemi, “Mimi...”

234 Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki wewe, wewe. Mungu akubariki, huko nyuma

kabisa. Mungu akubariki wewe, wewe. Mungu akubariki, huko nyuma. “Sasa naamini.” Mungu awabariki. Mungu ambariki yule mtu huko nyuma. Sasa, kumbukeni, sio *hapa* bali moyoni mwako, kwa Mungu, unafanya maungamo ya hadharani, “Bwana, ninajua ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Nimekwisha.”

²³⁵ Hivi majuzi nilikuwa nikizungumza na maskini rafiki yangu hapa mjini, Daktari Sam Adair. Tulikuwa tumeketi ofisini. Nikasema, “Sam, nimekuwa na kiungulia.”

Kasema, “Unajua ni kiungulia? Karibu na moyo wako?”

Nami nikasema, “Naam.”

²³⁶ Kasema, “Hiyo huenda ikawa ni mvilio tu moyoni—moyo—moyo—ugonjwa wa moyo—ugonjwa wa moyo.” Kasema... (Samahani.) Kasema, “Huenda ikawa ni ugonjwa wa moyo.”

²³⁷ Kasema, “Sasa, unajua upo?” Akasema, “Hebu nikuangalie.”

Akanifanyia uchunguzi, kasema, “La, huna tatizo lolote.”

²³⁸ Nikasema, “Sam, wakati wowote kinapokuja . . .” Nina umri wa miaka hamsini na miwili, naye Sam amenishinda kidogo kwa umri. Nikasema, “Kinapokuja, Sam, miaka hii yote thelathini niliyoweka katika kujaribu kuwafanya watu wamwamini Yesu Kristo, na Yule ambaye ninampenda na nimemfanyia kazi wakati huu wote; hailleti tofauti yoyote kwangu wakati Yeye atakapokuja, nitaenda Nyumbani.”

²³⁹ Akasema, “Billy, unajua, ninapopata yangu iliyo kuu kuliko yote? Ni kufanya jambo kwa ajili ya mtu mwingine.”

Nikasema, “Hayo ndiyo maisha halisi.”

²⁴⁰ Kama una urithi hapa katika ulimwengu huu, rafiki, ni urithi unaoharibika. Bali tunaupokea urithi usionyauka. Mwana mpotevu aliondoka akauacha urithi wake, naye akachukua sehemu yake akaenda nayo. Aliporudi, urithi wake—urithi wake ulikuwa umechafuliwa. Lakini kama umeutoroka wako, sivyo ilivyo kwa Ufalme wa Mungu, tunapokea urithi usioharibika. Hivi hutaki kuupokea Huo? Kumekuwako na yapata kumi na watano walioinua mikono yao, wenye dhambi waliotaka kuupokea urithi wao asubuhi ya leo. Huenda kuna mwingine kabla hatujaomba? Naam.

Polepole sana sasa:

Nampenda, na . . .

Amua sasa. Iwapo unajisikia inakupasa, huu ungekuwa ndio wakati.

Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu

Juu . . . (Mungu awabariki.

Mungu

awabariki . . . ? . . .)

²⁴¹ Baba wa Mbinguni, katika unyamavu wa wakati huu, tunakuletea Wewe kusanyiko hili, chini ya hali ya kudhoofisha asubuhi hii, Bwana, nikijaribu kuuleta Ujumbe huu kwa watu kwa sababu ninawapenda. Ninawataka wausikie, Bwana. Ninawataka watiwe nanga. Ninawataka wajue ya kwamba mambo haya yote ambayo yamefanywa katika miaka hii michache iliyopita hayajafanyika kwa bahati tu, imekuwa ni Wewe, Bwana. Wewe ndiwe umekuwa ukiyafungua mambo haya. Na, Ee Mungu, sote tunajisikia ya kwamba moja kwa moja mbele zetu kunayo Yubile kuu.

²⁴² Ninaomba kwa ajili ya hawa walioinua mikono yao. Wanajua wamekosea, Bwana. Mambo mengi madogo . . . Labda wamerithi pesa kidogo mara chache kutoka kwa mtu fulani, lakini zilifanya nini? Hawakujua mahali zilipoenda, wamesalia na kidogo tu, maana huo ni urithi uharibikao. Na kama wataziachia mtu mwingine, zitaharibika tena.

²⁴³ Lakini tunao urithi usioharibika, huo ni, wokovu, ukombozi, kurudi kwenye bustani ya Edeni tena. Liwazie hilo, Bwana, ni nani asingetaka kurudi kama vile Adamu na Hawa na kuishi kule nyuma? Chakula chetu kikitolewa kila siku; Baba wa Mbinguni sikuzote akiwa kwenye mburuzo akisema nasi; tukiiona ile Nuru kuu ikienda mbele zetu. Simba na mbwa mwitu wakila pamoja, fahali akila majani makavu, simba akila pamoja naye; wakati sasa wanalana, ama simba anamla fahali, na mbwa mwitu anamla fahali, chochote anachoweza kula. Lakini siku hizo haitakuwa hivyo. Wale ndege wakuu wazuri wakiruka. Hakutakuwako na huzuni. Kamwe hapatakuwa na alama kwamba tumeyapita matumaini yetu. Kote katika mburuzo kule tunawaona watoto wetu, wapendwa wetu. Ee Mungu, ni siku ya jinsi gani! Ni siku ya jinsi gani! Haidhuru tunapokea nini hapa duniani, yo—yo—yote yatanyauka, bali Hilo halitanyauka.

²⁴⁴ Mungu, huenda nisiweze kuzungumza na watu hawa walioinua mikono yao, hapa kwenye dunia hii. Sijui. Ninatumaini nitaifanya hivyo. Lakini nisipofanya hivyo, basi, Bwana, jalia nikutane nao kwenye ule mburuzo kule. Huenda wakasema kitu kama hiki, “Ndugu Branham, unakumbuka huko chini ardhini kabla jambo hili kuu halijatukia, asubuhi moja ulikuwa ukizungumza juu ya ku—kule kufunguliwa kwa ile mihuri iliyokuwa imewekwa kwenye Chombo cha udongo? Ilikuwa ni wakati huo ambapo Yeye alikuja katika chombo changu cha udongo, mimi ni mmoja niliyeinua mkono wangu asubuhi hiyo. Loo, nina furaha sana ya kwamba nilikuwa kule.”

²⁴⁵ Nitasema, “Ndugu, dada, nina furaha sana ya kwamba nilikuwa huko, pia. Sasa tuna ushirika pamoja kupitia kwenye nyakati zote.”

²⁴⁶ Wabariki, Baba, wao ni Wako. Wewe ulisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba. Na wote anaonipa

Baba watakuja, hakuna mmoja wao atakayepotea.” Kwa hiyo tuna—tunashukuru, Baba, kwa ajili ya hilo. Jalia waje sasa na kupata arabuni ya wokovu wao, sio kwenda kujiunga na kanisa. Lakini arabuni sio kujiunga na kanisa bali ni Kuzaliwa upya, kumpokea Roho Mtakatifu. Jalia wakupokee Wewe, Baba. Kwa kuwa tunalikabidhi mikononi Mwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁴⁷ Kwa ajili ya lesio hizi: Bwana Yesu, ninaombea lesio hizi; na kuomba ya kwamba Wewe utawabariki wote walio na haja, wote waliopo hapa, Bwana, maskini mwanamke huyu anayeketi hapa kwenye kiti cha magurudumu.

²⁴⁸ Baada ya mkutano huu mkuu asubuhi ya leo, Baba, kumhisi Roho Wako Mtakatifu akitujaza kabisa, tukilisikia Neno likishuka chini katika kilindi na kupata mizizi mioyoni mwa hawa watu. Kamwe hawatalisahau, Bwana. Kila wakati wanapoyasikia mambo haya watawazia ile mihuri ikifunguliwa. Sasa, tujalie kujua hiyo mihuri ilikuwa ni nini, Bwana, kusudi kila mmoja asitatanishwe niani mwake, bali atajua kutokana na “BWANA ASEMA HIVI” kwamba ni muhuri wa Mungu, ile mihuri ambayo Mungu alitufunulia.

²⁴⁹ Tunaomba ya kwamba Wewe utawaponya wagonjwa wote na wanaoteseka. Tujalie, Bwana. Roho Wako yupo. Kama unaweza kumwokoza mwenye dhambi huko nyuma upande wa nyuma ya hili jengo, unaweza kumponya mgonjwa huko, pia. Ninaomba ya kwamba Wewe utalijalia, Bwana, na kuwaponya wale ambao lesio hizi zinawakilisha ambao hawangeweza kufika hapa leo. Tunayakabidhi yote Kwako katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

²⁵⁰ Ninaamini ya kwamba wana mtoto mchanga anayetaka kuwekwa wakfu. Mwanamke huyo yuko hapa pamoja na huyo mtoto mchanga? Waweza kumleta hapa kwenye wakati huu? Tungefurahia kumweka wakfu jamaa huyo mdogo. La, si lazima awe mdogo, wewe njoo tu. (Baadhi ya wazee njoni msimame pamoja nami mkipenda wakati huu.) Yuna umri gani? Miaka miwili na nusu. Jina lake ni nani? Scott? Scott Ford, maskini Scott Ford, umri wa miaka minne na nusu, anataka kuwekwa wakfu asubuhi ya leo kwa Bwana na Mwokozi wake, Yesu Kristo. Mama yake anamleta. (Moja kwa moja, njoo huku, ndugu.)

²⁵¹ Bwana wa rehema, tunakuletea mtoto huyu mchanga asubuhi ya leo, kwa njia ya kuwekwa wakfu. Tukiweka mikono yetu juu ya mtoto huyu mchanga, mvulana huyu mdogo, na kuomba ya kwamba nguvu zilizomfufua Yesu kutoka kaburini zitamhuisha mvulana huyu mdogo. Mungu, jalia aishi katika afya na nguvu. Jalia aishi, Bwana, kwa utukufu Wako. Jinsi ambavyo tayari umeingia kumsaidia mtoto huyu mchanga, nasi tunakushukuru kwa ajili ya hilo. Nami ninaomba ya kwamba Wewe utaendelea kuwa pamoja na jamaa huyu mdogo.

Uwe na wazazi wake, wapendwa wake. Jalia...tunajua na tumefundishwa ya kwamba mambo yote yanatendeka kwa manufaa ya wale wampendao Bwana. Jinsi ambavyo mambo haya wakati mwingine huwavuta watu karibu na Wewe. Ninaomba ya kwamba Wewe utatujalia baraka tuombazo. Na sasa, Baba, katika utii wa Neno Lako, tunamkabidhi mvulana huyu mdogo Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Naomba uipokee maskini roho yake, nafsi, na mwili, na ukamtumie kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

²⁵² Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, mtoto Scott. Jinsi tunavyomshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo!

²⁵³ Sasa, ni nani atakayebatizwa? Kuna kundi la watu watakaobatizwa, ninaamini. Wakati tukijitayarisha kwa ajili ya jambo hilo, hebu na tuimbe...Hebu niwaambie kile huenda tukafanya, hebu na tuimbe...Nitamwacha Ndugu Neville afanye hivyo. Ninajua itakuwa ni sawa basi. Vema, bwana, Ndugu Neville.

²⁵⁴ Mnampenda Bwana, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mtaniombea? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Amina. Amina.



UFUNUO, MLANGO WA TANO SEHEMU YA II SWA61-0618

(Revelation, Chapter Five Part II)

MFULULIZO WA UFUNUO WA YESU KRISTO

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 18 Juni, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org